MAADHIMISHO YA MIAKA 50 YA UHURU WA TANZANIA BARA

1961 – 2011

MKOA WA KILIMANJARO

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,

S.L.P. 3070,

MOSHI.

Fax: 027-27-53248/027-27-51381

E-mail: raskilimanjaro@pmoralg.go.tz

Website: www.kilimanjaro.go.tz

TAARIFA YA MKOA WA KILIMANJARO KATIKA MAADHIMISHO YA MIAKA 50 YA UHURU WA TANZANIA BARA (1961 – 2011)

1.1 Utangulizi

Mkoa wa Kilimanjaro upo Kaskazini Mashariki mwa Tanzania Bara na upande wa Kaskazini umepakana na Jamhuri ya Kenya, upande wa Kusini Mashariki mkoa wa Tanga, upande wa Magharibi mkoa wa Arusha na Kusini Magharibi mkoa wa Manyara. Mkoa umeinuka kutoka tambarare hadi kufikia kilele cha Mlima Kilimanjaro chenye urefu wa mita 5895 juu ya usawa wa bahari, mlima mrefu kuliko yote katika Afrika na wenye theluji kwa kipindi chote cha mwaka.

1.2 Eneo la mkoa

Mkoa wa Kilimanjaro una kilomita za mraba ***13,209*** ambazo zimegawanywa kama ifuatavyo:- ardhi inayofaa kwa kilimo ni kilomita za mraba ***6,433*** sawa na asilimia ***48.7***, hifadhi ya wanyama kilometa za mraba ***3,051*** sawa na asilimia ***23.1***, misitu kilometa za mraba ***1,403*** sawa na asilimia ***10.6,*** mbuga za malisho kilometa za mraba ***2,018*** sawa na asilimia ***15.3*** na maji na vilima kilometa za mraba ***304*** sawa na asilimia ***2.3.***

1.1 Mgawanyo wa maeneo ya Utawala

Mkoa una wilaya ***6,*** Halmashauri ***7***, Tarafa ***30,*** Kata ***153,*** Vijiji ***472*** na Mitaa ***60*** katika Manispaa ya Moshi na vitongoji ***2,091***.

1.2 Idadi ya Watu

Mkoa ulikuwa na takriban watu ***300,000*** wakati tunapata Uhuru mwaka 1961. Idadi ya wakazi wa Kilimanjaro iliendelea kuongezeka na kulingana na sensa ya mwaka 1967 idadi ya wakazi ilikuwa ***652, 722***, sensa ya mwaka 1978 idadi ya wakazi iliongezeka hadi watu ***902,437,*** sensa ya mwaka 1988 idadi ya wakazi ilifikia 1,104,673, na kwa mujibu wa sensa ya Taifa ya watu na makazi ya mwaka

2002, idadi ya watu iliongezeka hadi kufikia ***1,381,149*** kukiwa na wastani wa ongezeko la watu la ***1.6%*** kwa mwaka na wastani wa msongamano wa watu (Population Density) wa watu ***104*** kwa kilometa ya mraba.



1.3 Pato la Mkoa

Pato la Mkoa limeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na uwepo wa shughuli za kilimo, biashara, utalii, ufugaji na uzalishaji viwandani. Wastani wa pato la mkazi wa mkoa huu wakati tunapata uhuru mwaka 1961 hadi miaka ya 1980 lilikuwa la kuridhisha kutokana na kuimarika kwa bei ya kahawa katika soko la dunia. Miaka ya 1990 bei ya kahawa iliporomoka katika soko la dunia hali iliyowalazimu wakulima wa kahawa wa mkoa huu kukata mibuni yao na kuotesha mazao mengine. Katika kipindi cha 2000 – 2010 kufuatia bei ya kahawa kuimarika pato la mkoa limeongezeka kutoka ***TShs. 290,517*** million hadi kufikia ***Tshs.1,184 Billion***, ambapo wastani wa pato la mkazi limeongezeka kutoka

Tshs.147,205 kwa mwaka 2000 hadi kufikia **Tshs.755,037** mwaka 2010 ikiwa ni juu ya wastani wa pato la mkazi kitaifa la **Tshs. 627,787/=.**

Kiuchumi, mkoa ulikuwa kwenye nafasi ya 17 Kitaifa kwenye miaka ya 1990 lakini kufuatia bei ya kahawa kuimarika tena, kuongezeka kwa shughuli za kitalii na uwekezaji mpya mkoa umepanda hadi kufikia nafasi ya 5 Kitaifa.

Makusanyo ya mapato/maduhuli ya Serikali

Mkoa umeendelea na juhudi za kukusanya kodi ya mapato na maduhuli mengine ya Serikali kwa ufanisi mkubwa. Mwaka 2005/2006 Mamlaka ya Mapato (TRA) ilikusanya **Tshs.38.9 bilioni** na kuongezeka hadi kufikia **Tshs.73.658 bilioni** mwaka 2010/2011. Kwa upande wa Halmashauri za wilaya na Manispaa makusanyo kutoka vyanzo vya ndani vya mapato ya Halmashauri yameongezeka kutoka **Tshs.2.24 bilioni** mwaka 2005/2006 na kufikia **Tshs.4.42 bilioni** mwaka 2010/2011.

1.4 Hali ya Ulinzi na Usalama

Baada ya Uhuru, uwepo wa viongozi wa jadi, "**Wamangi", "Wafumwa, "Wachili**" na viongozi wa ngazi za Mitaa ulisaidia sana kuimarisha hali ya ulinzi na usalama miongoni mwa wananchi. Kufuatia kufutwa kwa viongozi wa jadi/kimilia mwaka 1965 suala la ulinzi na usalama wa wananchi lilichukuliwa na Jeshi la Polisi.

Vyombo vya ulinzi na usalama vimeendelea kudhibiti matukio ya uvunjifu wa amani kikamilifu bila kuathiri shughuli za kawaida za wananchi wa mkoa huu hasa wale wanaoishi maeneo ya mipakani na mijini. Miaka ya hivi karibuni mkoa umekumbwa na matatizo ya wahamiaji haramu kutoka nchi za Somalia na Ethiopia, biashara ya madawa ya kulevya na magendo ya mpakani. Matukio haya yanatokana na muingiliano wa wananchi katika mpaka na nchi jirani ya Kenya na kusababisha uwepo wa matukio ya wizi, ujambazi na biashara ya magendo mpakani hasa kwenye miaka ya 1970 na 1980. Hata hivyo, mkoa kupitia vyombo

vya ulinzi na usalama umeendelea kuwashirikisha wananchi kudhibiti uhalifu kupitia dhana ya ulinzi shirikishi.

1.5 Hali ya Siasa

Tulipopata uhuru mwaka 1961 tulikuwa chini ya mfumo wa vyama vingi vya siasa. Vyama vya siasa vilivyokuwepo Kilimanjaro ni pamoja na TANU, UTP, African Congress na UMNUT. Serikali iliendelea kuheshimu utawala wa **Wamangi na Wafumwa** hadi mwaka 1964. Tuliendelea kuwa chini ya uongozi wa chama kimoja kuanzia mwaka 1965 hadi mwaka 1992 tulipoingia tena katika mfumo wa vyama vingi.

Kwa ujumla hali ya siasa mkoani Kilimanjaro ni nzuri ambapo katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba 2010 jumla ya vyama vya siasa 12 vilishiriki ambavyo ni CCM, CHADEMA, TLP, UPDP, APPT Maendeleo, SAU, UDP, DP, JAHAZI ASILIA, CUF na NCCR – Mageuzi. Mkoa wa Kilimanjaro una majimbo tisa ya uchaguzi ambayo ni Same Magharibi, Same Mashariki, Mwanga, Rombo, Vunjo, Moshi Vijijini, Moshi Mjini, Hai na Siha.

Katika Uchaguzi Mkuu wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro wameendelea kuonyesha imani yao kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kukipa ridhaa ya kuongoza nchi ambapo kwa upande wa U-Rais CCM ilipata asilimia 61.0; CHADEMA asilima 36 na vyama vilivyobaki tisa asilimia 3.0. Kwa upande wa majimbo, CCM ilipata majimbo 5 CHADEMA majimbo 3 na TLP jimbo 1.

Demokrasia katika Serikali za Mitaa kwa maana ya Halmashauri ni kuwa kati ya Halmashauri 7 za mkoa wa Kilimanjaro; Halmashauri 5 zinaongozwa na CCM na zilizobaki 2 zinaongozwa na CHADEMA. Mahusiano kati ya Madiwani na wataalam katika Halmashauri zote ni mazuri na ya kuridhisha. Changamoto zinazokabili uendeshaji katika Halmashauri ni uelewa mdogo wa kanuni za uendeshaji kwani asilimia kubwa ya Madiwani ni wapya na hivyo mkoa unajipanga kuwapa mafunzo ya mara kwa mara.

2.0 MUUNDO WA MKOA KUANZIA 1961 HADI 2011

Mkoa umeendelea kukua kutoka wilaya 2 za Moshi na Pare mwaka 1963 hadi kufikia wilaya 6 mwaka huu 2011. Mnamo mwaka 1972 wilaya ya Moshi iligawanyika mara mbili na kupata wilaya za Moshi na Rombo, ambapo mwaka 1975 wilaya ya Moshi iligawanyika tena na kupata wilaya ya Moshi na Hai. Mwaka 1979 wilaya ya Pare iligawanyika na kupata wilaya za Same na Mwanga, aidha, wilaya ya Hai iligawanyika mwaka 2005 na kupatikana wilaya za Hai na Siha. Katika mtiririko huo mkoa ulikuwa na Halmashauri tatu za Pare, Kilimanjaro na Mji wa Moshi wakati tunapata Uhuru na sasa zimeongezeka hadi kufikia Halmashauri 7. Mkoa una Tarafa 30, Kata 153, Vijiji 472, Vitongoji 2,091 vya Halmashauri za wilaya na Mitaa 60 katika Manispaa ya Moshi.

3.0 MAJUKUMU YA MKOA

Mkoa wa Kilimanjaro umeendelea kutekeleza majukumu yake ya kumhudumia mwananchi tangu ulipoanzishwa Aprili, 1963. Tangu kuanzishwa mkoa mwaka 1963 hadi mwaka huu 2011, majukumu yake kimsingi yamejikita kama ifuatavyo:

(i) Kusimamia, kuendeleza na kusukuma maendeleo ya wananchi na asasi mbalimbali za mkoa kiuchumi, kisiasa na kijamii kupitia ngazi mbalimbali za utawala za wilaya na Halmashauri kwa kushauri, kuelekeza na kuelimisha.

(ii) Utekelezaji wa majukumu yake katika kipindi cha mpito 1961 hadi 2011 umepitia sera, mabadiliko na mifumo mbalimbali ya kiutawala ikiwemo ifuatayo:

   (a) Serikali za mitaa 1963 hadi 1972,

   (b) Kuvunjwa kwa serikali za mitaa na madaraka mikoani 1972 hadi 1984,

   (c) Kurudishwa Serikali za mitaa 1984 hadi sasa 2011,

   (d) Uanzishwaji wa Sekretarieti za mikoa 1998 hadi 2011.

Katika kuboresha huduma zake mkoa umejipangia Dira, Dhima na Majukumu kama ifuatavyo:-

Dira: Kuwa Sekretarieti inayoongoza kwa kutoa huduma bora za ushauri na utaalamu kwa serikali za mitaa na wateja wengine.

Dhima: Kuhakikisha kuwa ushauri wa kitaalam unatolewa kwa viwango na ubora wa hali ya juu kwa Halmashauri za Wilaya na wateja wengine kwa lengo la kukuza na kuboresha maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Katika kutekeleza Dira na Dhima hizo mkoa umejipangia majukumu yafuatayo:-

i) Kusimamia amani na utulivu.
ii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa sera zilizoainishwa na Wizara/Sekta mbalimbali za Serikali.
iii) Kuzijengea Halmashauri na sekta binafsi mazingira ya kuziwezesha kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa;
iv) Kusimamia utawala bora kwa Halmashauri na jamii.
v) Kufuatilia na kutathmini miradi ya maendeleo ya Halmashauri na utoaji wa huduma za jamii.
vi) Kutoa ushauri kwa sekta na miradi husika ikiwa ni pamoja na kutafuta wawekezaji ili kuinua uchumi wa wananchi na mkoa kwa ujumla.

4.0 HALI YA UONGOZI NA UTAWALA KUANZIA MWAKA 1961 HADI 2011

Kabla ya uhuru Wakuu wa Mikoa walijulikana kama Wakuu wa Majimbo "Provincial Commissioners" lakini baada ya uhuru walijulikana kama Wakuu wa Mikoa "Regional Commissioners". Wakati Tanzania Bara (Tanganyika) inapata Uhuru wake tarehe 09.12.1961 mkoa wa Kilimanjaro ulikuwa sehemu ya Jimbo la Kaskazini (Northern Province) na makao makuu yalikuwa Arusha na lilikuwa likiongozwa na **Mheshimiwa PC Edward Barongo** hadi Aprili 1963 mkoa ulipoanzishwa rasmi, ambapo **Mheshimiwa Peter Kisumo** alichaguliwa kuwa Mkuu wa kwanza wa Mkoa.

Katika kipindi cha 1963 hadi 2011 mkoa umeongozwa na Wakuu wa Mikoa 18 katika vipindi tofauti kama ifuatavyo:-

Na	Jina	Mwaka
1	Mhe. PC Edward Barongo	1961 – April, 1963
2	Mhe. Peter Kisumo	April 1963- Oktoba,1965
3	Mhe. Louis P.D. Ngua	Oktoba 1965 - 1967
4	Mhe. Balozi Juma Majid	1967 - 1969
5	Mhe. Louis P. Sazia	1969 - 1972
6	Mhe. J.D. Namfua	1972 - 1973
7	Mhe. Peter Kisumo	1973 - 1975
8	Mhe. Lawi N. Sijaona	1975 – Oktoba 1980
9	Mhe. PC Edward Barongo	Oktoba 1980 – Februari 1983
10	Mhe. Pius Msekwa	Februari 1983 – April 1984
11	Mhe. Paul P. Kimiti (Mb)	April 1984 – 1989
12	Mhe. J.W. Kasubi	1989 -1990
13	Mhe. Zakhia H. Meghji	1990 – 1991
14	Mhe. Samwel J. Sitta (Mb)	1991 – Mei 1993
15	Mhe. Gallus N. Abeid	Mei 1993 – Desemba1995
16	Mhe. Prof. Joseph Mbwiliza (Mb)	Desemba 1995 – April 1998
17	Mhe. Prof. Philemon Sarungi (Mb)	April 1998 – Agosti 2000
18	Mhe. Cynthia Hilda Ngoye (Mb)	Agosti 2000 – Machi 2006
19	Mhe. Mohammed A. Babu	Machi 2006 – April 2009
20	Mhe. Monica Ngenzi Mbega (Mb)	April 2009 – Agosti 2010
21	Mhe. Meja Generali Said S. Kalembo	Agosti 2010 - 2011

Wakati tunapata uhuru Makatibu Tawala walijulikana kama "Administrative Secretaries" kati ya mwaka 1961 – 1972 na baadaye Wakurugenzi wa Maendeleo wa Mikoa (Regional Development Directors - RDDs) kwa upande wa mikoa; na Wakurugenzi wa Maendeleo wa Wilaya (District Development Directors – DDDs) kwa upande wa wilaya. Kutokana na muundo mpya wa Tawala za Mikoa na

Serikali za Mitaa; Makatibu Tawala wa Mikoa (Regional Administrative Secretaries – RAS) walirudishwa tena kufuatia maboresho yaliyofanyika kwa mujibu wa Sheria Na.19 ya mwaka 1997 iliyoanzisha upya Sekretarieti za Mikoa (Regional Secretariets).

Orodha ya Makatibu Tawala /Wakurugenzi wa Maendeleo wa Mkoa kwa vipindi hivyo ni kama ifuatavyo:-

Na	**Jina**	**Mwaka**
Makatibu Tawala wa Mkoa (RAS)		
1	Bw. K.M. Kikwete	1963 - 1966
2	Bw. Sebastian Bunjoro	1966 - 1969
3	Dr. Cuthbert Hatibu	1969 - 1972
Wakurugenzi wa Maendeleo wa Mkoa (RDD)		
4	Bw. Sylvester Barongo	Julai 1972 - 1973
5	Bw. J.A.T. Muwowo	1973 - 1974
6	Bw. Daudi Semkiwa	1974 - 1978
7	Dr. Bismark Mwansasu	1978 - 1980
8	Bw. J. A.T. Muwowo	1980 – 1983
9	Bw. Raphael Mhagama	1983 – 1985
10	Bw. S.K. Masinde	Sept.1985 – Mei 1986
11	Bw. Godwin Mgendi	Mei 1986 – 1988
12	Bw. Julius Semwaiko	1988 - 1995
Makatibu Tawala wa Mkoa (RAS)		
13	Bw. Paul O. Chikira	1995 - 2004
14	Bibu Ndeshukurwa Abel Sumari	2004 - 2007
15	Bibi Hilda Ausi Gondwe	2007 - 2011

5.0 SERA NA SHERIA ZILIZOKUWEPO TANGU 1961 NADI HIVI SASA

Wakati tunapata uhuru mwaka 1961, tulikuwa tunaongozwa na sera na sheria mbalimbali ambazo ziliandaliwa kitaifa na kutekelezwa na mikoa yote. Baadhi ya sera na sheria hizo tulizirithi toka utawala wa kikoloni na tuliendelea kubadilisha sera na sheria kulingana na mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Wakati wote tuliongozwa na kaulimbiu ya **Uhuru na Kazi**.

- Sheria ya kuanzishwa kwa Tarafa mwaka 1963,
- Sheria ya kufuta mfumo wa vyama vingi vya siasa na kuwa na mfumo wa chama kimoja cha siasa mwaka 1965,
- Kuanzishwa kwa sera ya Azimio la Arusha iliyowezesha umilikaji wa njia kuu za uchumi na kuanzishwa kwa vijiji vya Ujamaa mwaka 1967. Mwaka 1969 mkoa wa Kilimanjaro ulikuwa na vijiji vya Ujamaa 11,
- Kuanzia mwaka 1964 – 1969 ulianzishwa Mpango wa Maendeleo ya miaka mitano,
- Mkoa uliridhia Tamko la Taifa la kuimarisha mihimili tisa ya miji ya maendeleo ya mwaka 1969,
- Kufutwa kwa serikali za mitaa mwaka 1972 na kuanzishwa kwa Madaraka mikoani,
- Kuanzishwa kwa sheria ya vijiji vya Ujamaa mwaka 1975,
- Kurudishwa kwa serikali za mitaa za mwaka 1982 na kuundwa kwa sheria namba 7 na 8,
- Kuanzishwa kwa Universal Primary Education (UPE) kulikowezesha kuandikisha wanafunzi wengi wa shule za msingi kwa kuongeza madarasa, shule, na idadi ya walimu, Kuanzishwa rasmi kwa elimu ya watu wazima ambayo iliwezesha wananchi wengi ambao hawakuwahi kwenda shule kuweza kujiunga na elimu hiyo na kuinua kiwango cha elimu katika mkoa,
- Mwaka 1976 vilifutwa vyama vya ushirika kulikopelekea kushuka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara,
- Mwaka 1982 kurejeshwa tena kwa vyama vya ushirika, na kuundwa kwa sheria ya vyama vya ushirika mwaka 1982,

- Mwaka 1983 kuundwa kwa sheria ya wahujumu uchumi ambapo baadhi ya wafanyabiashara ambao walitiliwa mashaka juu ya uhalali wa biashara zao waliwekwa kizuizini na kuathiri uchumi,
- Mwaka 1992 kuanzishwa upya mfumo wa vyama vingi vya siasa ambapo vyama tisa vya siasa vilianzishwa mkoani na hadi sasa viko vyama kumi na moja,
- Mwaka 1995 ilianzishwa sheria ya ubinafsishaji wa mashirika ya umma ikiwa ni pamoja na mashamba makubwa ya kahawa, ngano, mkonge ambapo ilituathiri sana kiuchumi,
- Kuanzishwa kwa sheria Na.17 ya mwaka 1997 ambayo ilianzisha Sekretarieti za Mkoa.

6.0 MABADILIKO NA MATUKIO MAKUU KATIKA MFUMO WA KISIASA, KIULINZI, KIUTAWALA, KIUCHUMI, KITEKNOLOJIA NA KIJAMII.

Mkoa wa Kilimanjaro umejengeka katika misingi imara ya utawala wa jadi chini ya viongozi wa kimila yaani **"Wamangi", Wafumwa** na **"Wachili";** serikali kuu na zile za mitaa katika vipindi tofauti kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na baada ya nchi yetu kupata Uhuru. Kabla Wakoloni wa Kijerumani hawajaingia nchini, viongozi wa kimila walitawala wakisaidiwa na "Mabaraza ya Wazee" katika kufikia na kutoa maamuzi katika mashauri mbalimbali yaliyohusu jamii zao. Kuingia nchini kwa utawala wa Kirejumani kwenye miaka 1880's hawakutaka kutambua utawala wa kijadi na hivyo viongozi wa kijadi walianza kupambana nao akiwemo Mangi Sina aliyekuwa anatawala maeneo ya Kibosho.

Aidha, katika vita kuu ya pili ya dunia (1914 – 1918) Ujerumani ilishindwa na Waingereza ambao baadaye walitawala nchi yetu na kutambua viongozi wa jadi na kuwaingiza kwenye mfumo wa utawala. Utawala wa Kiingereza ulipitisha sheria ya Mamlaka za Wenyeji Sura Na.72 ya mwaka 1926 ambayo kwa mkoa wa Kilimanjaro ilikuwa chimbuko la kuanzishwa kwa serikali za mitaa ambapo Halmashauri za Mji wa Moshi, Kilimanjaro (KDC) na Pare zilikuwa kati ya Halmashauri 47 zilizokuwa zimeanzishwa mwaka huo.

Wakati Tanzania Bara (Tanganyika) inapata Uhuru mkoa wa Kilimanjaro ulikuwa sehemu ya Jimbo la Kaskazini (Northern Province) na Jimbo la Tanga (Tanga Province) na ulianzishwa rasmi April 1963 kwa kuunganisha wilaya za Moshi (kutoka Jimbo la Kaskazini) na wilaya ya Pare (kutoka Jimbo la Tanga) na ulikuwa na Halmashauri mbili za Kilimanjaro (KDC) na Pare.

6.1 Kuanzishwa kwa Tarafa 1965

Katika sheria iliyounda mikoa, iliunda pia ngazi za chini za utawala zikiwemo Wilaya, Tarafa na Kata na kufuta jina la "Division" lililokuwa linatumika wakati wa Ukoloni. Mfumo wa utawala ngazi ya Tarafa na Kata ulianza rasmi 1965, ambapo mkoa wa Kilimanjaro uligawanywa katika Tarafa 22 zikiongozwa na viongozi walioitwa "Division Secretary" au "Assistant District Commissioners".

Mgawanyo wa Tarafa hizo ulikuwa kama ifuatavyo:-

Wilaya ya Moshi/Kilimanjaro: Vunjo Mashariki, Vunjo Magharibi, Kibosho, Hai Mashariki, Moshi Mjini, Lyamungo, Machame, Masama, Siha, Useri, Tarakea na Mashati.

Wilaya ya Pare: Gonja, Same, Mamba Vunta, Mwembe, Mbaga, Suji, Ndungu, Usangi, Ugweno na Lembeni.

Mabadiliko ya maeneo ya kiutawala katika kuanzisha Tarafa yalizingatia kwa kiasi kikubwa maeneo ya kiutawala ya jadi yaliyokuwa chini ya ***"Wamangi"*** kwa upande wa Uchaggani na ***"Wafumwa"*** kwa upande wa Upareni.

6.2 Kuanzishwa kwa Azimio la Arusha mwaka 1967

Mkoa wa Kilimanjaro ni miongoni mwa mikoa iliyoshuhudia kuundwa kwa Azimio la Arusha mwaka 1967 lililokuwa limelenga kuanzisha siasa ya Ujamaa na Kujitegemea; sambamba na kutaifisha njia kuu za uchumi ili zimilikiwe na umma kwa lengo la kuleta usawa miongoni mwa jamii ya Watanzania. Katika mkoa wa Kilimanjaro mashamba makubwa (Estates) 41, mabenki na nyumba kadhaa

zilizokuwa na thamani ya zaidi ya Sh. Million tano katika Mji wa Moshi zilitaifishwa.

6.3 Kuvunjwa kwa Mabaraza ya Halmashauri:-

Mnamo mwaka 1972 Serikali ilipovunja Mabaraza ya Halmashauri (Council) na kuanzisha Madaraka Mikoani, Mkoa wa Kilimanjaro uliathirika kimaendeleo hasa katika maeneo ya Mji wa Moshi, hadi ziliporejeshwa tena mwaka 1982.

6.4 Hali ya Kisiasa kabla na baada ya Uhuru

Wakati Tanzania Bara (Tanganyika) inapata Uhuru, Wachagga walikuwa na chama chao cha Siasa, Bendera yao iliyokuwa na Nembo maalum iliyojulikana kama **"Mbuya ya Wachagga"** na siku maalumu iliyojulikana kama **"Chagga Day"** iliyokuwa inasherehekewa tarehe **10 Desemba** kila mwaka. Kufuatia marekebisho ya Sheria ya kuondoa Mamlaka za Wenyeji Na.13/62 ya mwaka 1963, Wachagga walisitisha kutumia nembo yao, na kutumia zile za kitaifa.

Aidha, Chama cha TANU kilichoanzishwa tarehe 07.07.1954 chini ya uongozi wa Baba wa Taifa Mwalimu J.K. Nyerere kilichoongoza nchi hadi kufikia kupata Uhuru tarehe **09.12.1961** kilikuwa na wanachama wa kutosha kupambana na vyama vingine kama African Congress, UTP na UMNUT. Mkoa ulipitia kwenye huo mfumo wa vyama vingi hadi ulipoanzishwa rasmi mfumo wa utawala wa chama kimoja chini ya TANU mwaka 1965.

6.5 Kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi vya Siasa 1992

Mkoa wa Kilimanjaro ulipitia mabadiliko mbalimbali ya mifumo ya kisiasa kuanzia vyama vingi baada ya Uhuru Chama kimoja na baadaye vyama vingi mwaka 1992. Mfumo wa vyama umetoa uimarishaji demokrasia kwa kutoa fursa kwa wananchi wengi kuchagua viongozi na kuchaguliwa kupitia mfumo huu wa vyama vingi. Katika chaguzi mbalimbali vyama vilivyopo katika mkoa wa Kilimanjaro CCM, CHADEMA, CUF, APPF Maendeleo, NCCR Mageuzi na SAU

vimepata uwakilishi katika ngazi mbali mbali za uongozi katika Serikali za Mitaa, vitongoji, vijiji, kata na uwakilishi Bungeni.

6.6 Utekelezaji wa sera mbalimbali za kitaifa

Mkoa wa Kilimanjaro umekuwa mstari wa mbele katika kutekeleza sera mbalimbali za kitaifa ambazo zimechangia kukua kwa uchumi wa wananchi na mkoa kwa ujumla. Mwaka 1974 mkoa ulitekeleza sera ya **Thubutu** iliyolenga kuimarisha matumizi sahihi ya mabonde ya umwagiliaji ili kuboresha kilimo na kuongeza kiwango cha uzalishaji mazao, na mwaka 1976 mkoa ulishiriki katika sera ya **Siasa ni Kilimo**. Sera hii ililenga kusisitiza matumizi endelevu ya maji, utunzaji wa mazingira ambapo wananchi walishiriki kikamilifu kwa kuchimba **"ndiva" au malambo** kwa ajili ya kukusanya na kuhifadhi maji.

Mkoa ulishiriki kikamilifu katika Sera iliyolenga kutoa elimu ya msingi kwa wote "Universal Primary Education"- (UPE), Elimu ya Watu Wazima, "Operation Vijiji vya Ujamaa, kuanzisha maduka ya Ujamaa, Elimu ya Afya ya Msingi, Sera ya Maji, Ujenzi, Barabara n.k.



Rais Nyerere (katikati) alipofungua rasmi chanzo cha maji (in-take) Ruvu Mferejini Wilaya ya Pare mwaka 1973.

7.0 MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA SEKTA MBALI MBALI KUANZIA MWAKA 1961 HADI 2011

7.1 KILIMO:

Mkoa umegawanyika katika kanda za kilimo za tambarare na milimani ambapo kanda za milimani hulimwa mazao ya kudumu kama kahawa, migomba, miti na na kanda za tambarare hulima mazao ya msimu kama mahindi, maharage,fiwi, mpunga n.k. Kuanzia mwaka 1961 kilimo kimekuwa kikichangia zaidi ya asilimia 60 ya pato la mkoa. Asilimia 70 ya wakazi wa mkoa huu wanategemea kilimo kwa maisha yao, na zaidi ya asilimia 80 ya kilimo hicho hutegemea mvua. Eneo linalofaa kwa kilimo ni hekta 643,300 sawa na asilimia 48.7 ya eneo la mkoa na eneo kwa kaya ni wastani wa hekta 0.5 hadi hekta 1.5.

Msisitizo mkubwa wa kilimo mwanzoni ulikuwa wa zao la kahawa, pamba na mkonge ambayo ni mazao ya biashara. Wakulima wadogo walishauriwa kulima mazao ya biashara na kutumia fedha wanazopata kutokana na kuuza mazao hayo kujinunulia chakula. Kilimo cha mazao ya biashara kiliinua kipato cha wakulima na kuwawezesha kujijengea nyumba bora na kusomesha watoto wao.



Kuanguka kwa bei ya kahawa, mkonge na pareto katika soko la dunia kulisababisha mashamba ya kahawa kutotunzwa vizuri na vile vile wakulima wadogo walipanda nafaka kwenye maeneo ambayo hapo awali yalikuwa ni ya pamba na pareto.



Wastani wa mavuno ya mazao makuu mkoani kuanzia mwaka 1964 – 2010 yalikuwa kama ifuatavyo:-.

Na.	**Zao**	**Wastani wa mavuno (tani) 1964**	**Wastani wa mavuno (tani) 2010**
1.	Kahawa	17,460	8,440
2.	Pamba	9,675	101
3.	Mkonge	2,654	9,000
4.	Pareto	10,840	0
5.	Sukari	16,048	84,000
6.	Mahindi	40,086	342,970
7.	Mpunga	20,854	76,551
8.	Ngano	4,350	9,219
9.	Maharagwe	9,125	36,130
10.	Ndizi	287,711	1,029,280

Ongezeko la mavuno ya mazao ya chakula na biashara 1961-2011:

i) Mahindi kutoka wastani wa tani 1.3 hadi wastani wa tani 3.5 kwa hekta,
ii) Ndizi kutoka wastani wa tani 3.8 hadi wastani wa tani 12 kwa hekta,
iii) Mpunga kutoka wastani wa tani 2.0 hadi wastani wa tani 7.5 kwa hekta,
iv) Maharagwe kutoka wastani wa tani 0.5 hadi wastani wa tani 1.0 kwa hekta,
v) Kahawa kutoka wastani wa kilo 240 hadi wastani wa kilo 400 kwa hekta,
vi) Pamba kutoka wastani wa kilo 137 hadi wastani wa kilo 250 kwa hekta
vii) Sukari kutoka wastani wa tani 2.4 hadi wastani wa tani 11.4 kwa hekta

Mafanikio haya yanatokana na matumizi bora ya pembejeo na ushauri wa kitaalamu katika kilimo.

7.2 Kilimo cha umwagiliaji:

Shughuli za umwagiliaji katika kipindi hiki ziliendelezwa kwa ujenzi wa mifereji ya maji kwenye shamba la Kenaf, umwagiliaji wa miwa kwenye kiwanda cha sukari Arusha Chini (TPC), ujenzi wa mabwawa ya Kalimawe na Nyumba ya Mungu. Ukanda wa milimani mifereji ya asili 'mifongo' ilikuwa ikitumika kabla ya Uhuru. Maeneo makubwa ya umwagiliaji yalikuwa ni ekari 35,750 pamoja mifereji midogo ya asili ekari 1,610.

Shamba la Kenaf/TPC	-	ekari 25,000
Marwa - Same	-	ekari 50
Gunge – Hedaru	-	ekari 2,000
Bonde la Mkomazi	-	ekari 4,500
Ziwa Jipe/Butu	-	ekari 1,000

Eneo la umwagiliaji limeongezeka kutoka ekari 37,360 mwaka 1961 hadi ekari 134,688 mwaka 2011; ikiwemo pia miradi mikubwa ya umwagiliaji ya Lower Moshi na Ndungu yenye ukubwa wa hekta 4,300 (ekari 10,750).

7.3 Upatikanaji wa Pembejeo:

Mwaka 1961 matumizi ya mbegu bora, mbolea na viuatilifu yalikuwa madogo. Wakulima walikuwa wanajipatia pembejeo hizo kwenye maduka ya watu binafsi na vile vile kupitia vyama vya ushirika vya mazao kama KNCU, VUASU na Bodi ya Pamba kwa mkopo na kurudisha baada ya kuuza mazao. Mwaka 2011 pembejeo zinapatikana toka kwa wakala wa pembejeo ambao kwa sasa wapo 566 kutoka vyama vya msingi vitatu vilivyokuwepo. Matumizi ya mbolea yameongezeka hadi kufikia tani 16,050 mwaka 2011.

7.4 Huduma za Ugani:

Wakulima walikuwa wanapata elimu ya ukulima bora kutoka kwa wagani ambapo kwa kipindi hiki walikuwa wachache sana. Vyama vya msingi hasa vinavyoshughulika na zao la kahawa walitumia wagani wao kutoa elimu ya uzalishaji bora wa kahawa. Mwaka 2011 wapo wagani 576 wanaotoa elimu mbalimbali (kilimo, mifugo, umwagiliaji, ushirika). Maafisa Ugani wamepatiwa pikipiki 80 na kujenga nyumba 53 za watumishi. Wakulima wanaopatiwa ushauri ni wastani wa 1,382,310, na jumla ya mashamba darasa 1,023 yameanzishwa.

7.5 Hifadhi ya chakula:

Wakati wa Uhuru watu walikuwa wachache wakiwa na maeneo makubwa ya kilimo. Wananchi walikuwa wanahifadhi chakula kwa kutumia vifaa vya asili vikiwepo **vihenge na vibuyu**. Hata hivyo, watu walivyozidi kuongezeka na uzalishaji wa chakula pamoja na uharibifu wa mazao mfano dumizi kuingia mkoani miaka ya 70, vyakula vinahifadhiwa kwenye mapipa, vihenge na kutumia madawa. Maghala makubwa ya kuhifadhi chakula yameanza kujengwa sehemu mbalimbali mkoani kuanzia miaka ya 70 na 80.

Mwaka 2011 mkoa una maghala 167 yenye uwezo wa kuhifadhi tani 67,571 za mazao. Elimu ya hifadhi ya chakula kwa kutumia stakabadhi ya mazao ghalani inaendelea kutolewa. Hivi sasa vipo vyama 9 vya ushirika vyenye utaratibu huo kwa mazao ya mahindi na mpunga.

7.6 Changamoto:

Mkoa unakabiliwa na changamoto mbalimbali za uzalishaji kilimo kama ifuatavyo:-

i) Hali ya hewa inayobadilika badilika ambayo inaletwa na athari ya mabadiliko ya tabia nchi inayosababisha upungufu wa mazao kutokana na ukame.

ii) Ufinyu wa ardhi kwa ajili ya kuongeza eneo la kilimo.

iii) Matokeo ya utafiti kutotumiwa na wakulima.

iv) Bei kubwa ya pembejeo za kilimo, hivyo kusababisha matumizi kidogo.

7.7 Matarajio:

Mkoa utatumia fursa nyingi zilizopo za kuboresha kilimo ambazo ni pamoja na:- - kuwepo kwa wataalam wa kutosha wa ugani,

- wananchi kuwa na kiwango cha elimu cha kuridhisha,
- mawasiliano ya uhakika hadi katika vjijijini vingi vya mkoa weku,
- mawakala wa pembejeo wenye ujuzi na uzoefu wa kutosha,
- mkoa ni mkongwe katika ushirika na unapata huduma kutoka vituo 3 vya utafiti (TaCRI – Lyamungo, Selian, Tengeru).

Kwa kutumia fursa hizi pamoja na kuboresha kilimo cha umwagiliaji; kupanda mazao kufuatana na eneo; kuongeza matumizi ya pembejeo na kuongeza thamani ya mazao (Value Added) kwa usindikaji kutaboresha maisha ya wananchi, uchumi wa mkoa na taifa kwa ujumla.

8.0 Mifugo:

Mifugo huchangia zaidi ya asilima 16 katika pato la mkoa na zinahusisha ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, kuku, nguruwe, mbuzi na kondoo katika ukanda wa milimani, ambapo mifugo hufugwa ndani (zero grazing). Katika ukanda wa tambarare ufugaji wa ng'ombe wa nyama, mbuzi na kondoo ndiyo shughuli kubwa na mifugo hiyo inachungwa mbugani ikijitafutia chakula yenyewe (extensive grazing). Shabaha ya ufugaji ni kuwapatia wakulima wadogo maziwa, nyama na mbolea, pamoja na kuwaongezea kipato kutokana na kuuza maziwa na nyama katika masoko vijijini.

8.1 Mafanikio:

i) Idadi ya ng'ombe wa maziwa imeongezeka kutoka wastani wa ng'ombe 200 mwaka 1961 hadi kufikia zaidi ya ng'ombe 183,000 mwaka 2011 na wa kienyeji wameongezeka kutoka ng'ombe 338,700 mwaka 1961 hadi kufikia ng'ombe 365,733 mwaka 2011. Idadi ya madume bora ya maziwa imeongezeka kutoka 500 mwaka 1961 hadi 27,852 mwaka 2011

ii) Idadi ya mbuzi kwa ujumla imeongezeka kutoka 169,173 mwaka 1961 hadi mbuzi 575,577 mwaka 2011, wakati idadi ya kondoo wa maziwa imeongezeka kutoka 101,039 mwaka 1961 hadi kufikia 257,260 mwaka 2011 na idadi ya mbuzi wa maziwa wameongezeka kutoka 16 mwaka 1961 hadi 791 mwaka 2011.

iii) Idadi ya nguruwe imeongezeka kutoka 6,343 mwaka 1961 hadi 55,070 mwaka 2011.

iv) Majosho yanayofanya kazi yameongezeka kutoka 0 mwaka 1961 hadi 75 mwaka 2011 na malambo yanayofanya kazi yameongezeka kutoka 0 mwaka 1961 hadi 91 mwaka 2011.

v) Vituo vya mifugo vimeongezeka kutoka 0 mwaka 1961 hadi 53 mwaka 2011 na maduka ya pembejeo yameongezeka kutoka 0 mwaka 1961 hadi 125 mwaka 2011.

vi) Masoko na minada yameongezeka kutoka 0 mwaka 1961 hadi 10 (minada 2 ya Mpakani) mwaka 2011.

vii) Vituo vya uhamilishaji (Artificial Insemination) vimeongezeka kutoka 15 mwaka 1961 hadi 57 mwaka 2011 na idadi ya ng'ombe waliohamilishwa imeongezeka kutoka 579 mwaka 1961 hadi 3,240 mwaka 2011.

viii) Dawa za kuogesha mifugo zenye ruzuku ya Serikali zimeongezeka kutoka lita 0 mwaka 1961 hadi lita 32,874 mwaka 2011. Ambapo mwanzo serikali haikuwa na mpango wa kutoa ruzuku kwa ajili pembejeo za kilimo.

ix) Wapo wataalam 202 wanaotoa huduma za ugani na mashamba darasa ya ufugaji yameongezeka kutoka 0 mwaka 1961 hadi mashamba darasa 60 mwaka 2011. Idadi ya wafugaji waliopata mafunzo ya ufugaji bora imeongezeka kutoka 3,500 mwaka 1961 hadi 28,921 mwaka 2011.

x) Utengaji wa maeneo ya malisho ya mifugo umeongezeka kutoka vijiji 0 mwaka 1961 hadi vijiji 28 (Siha – vijiji 6, Hai – vijiji 4, Moshi – vijiji 8, Mwanga – vijiji 4, na Same vijiji 6) mwaka 2011.

xi) Uzalishaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita 68,870,830 mwaka 1961 hadi lita 110,00,000 kwa mwaka 2011. Viwanda vidogo 14 vya kusindika maziwa vimejengwa katika wilaya za Hai, Moshi (V) na Rombo na huzalisha zaidi jibini, siagi na maziwa lala (mtindi).

8.2 Mpango wa unywaji maziwa shuleni:

Tulipopata Uhuru mwaka 1961 hatukuwa na mpango wa unywaji maziwa shuleni. Mpango huu ulianzishwa mwaka 2006 kupanua soko la maziwa. Shule 7 za wilaya ya Moshi zenye watoto 2,200 na shule 6 za wilaya ya Hai zenye watoto 4,780 zinanufaika na mpango huu. Watoto hupatiwa maziwa mara mbili kwa wiki, siku moja ikigharamiwa na wazazi, na ya pili ikigharamia na wafadhili kutoka Australia na Italy.

8.3 Changamoto:

i) Uhaba wa ardhi, maji na malisho bora ya mifugo.

ii) Tija ndogo ya uzalishaji kutokana na aina za mifugo pamoja na mifumo ya uzalishaji iliyopo.

iii) Uhaba wa masoko ya mifugo na mazao yatokanayo na mifugo na vile vile viwanda vya kusindika mifugo na mazao yake.

iv) Ukosefu wa wataalam wa kutosha katika nyanja mbali mbali za mifugo.

8.4 Matarajio:

Mkoa umelenga kuinua pato la mfugaji kwa kufuga kisasa na kwa biashara kwa kuboresha huduma zote za mifugo, pamoja na miundo mbinu ikiwa ni pamoja na kuhamasisha unywaji wa maziwa shuleni ili kuongeza wigo wa soko la bidhaa za mifugo.

9.0 Uvuvi

Wakati tunapata Uhuru shuughuli za uvuvi zilikuwa zinafanyika kwa upeo mdogo sana hadi mwaka 1968. Bwawa la Nyumba ya Mungu lilipofunguliwa rasmi, vijiji vingi vilianzishwa kuzunguka bwawa hilo ambalo lilikuwa na ukubwa wa ***mita za mraba 56;*** na wakazi wake waliendelea kujihusisha na shughuli za uvuvi ambapo mwaka 1970 kulikuwepo na wavuvi wapatao 3,300 waliovua kiasi cha tani 28,402. Idadi ya wavuvi na kiasi walichovua kiliendelea kupungua mwaka hadi mwaka na hadi kufikia wavuvi chini ya 1,000 mwaka 1975 waliovua chini ya tani 4,000 kwa mwaka.

Aidha, shughuli za uvuvi zimeendelea katika mabwawa mengine ya Kalimawe, Chala, Jipe na kwenye baadhi ya mito mikubwa kama vile Kikafu, Pangani n.k. Idadi ya mavuno ya samaki katika vyanzo mbalimbali imeendelea kupungua mwaka hadi mwaka hadi kufikia tani 511 mwaka 2011 kutokana na uvuvi wa mfululizo usiotoa nafasi kwa samaki kuzaliana haswa katika Bwawa la Nyumba ya Mungu, ziwa Jipe kuvamiwa na magugu maji aina ya "TYPHA", uvuvi haramu wa kutumia baruti na zana haramu (makokoro), na mabadiliko ya tabia nchi yanaathiri upatikanaji wa maji ya kutosha.

9.1 Mafanikio:

Vikundi 14 vya usimamizi wa rasilimali za uvuvi (Beach Management Unit) vimeanzishwa na kupatiwa mafunzo katika maeneo ya vijijini vinavyozunguka bwawa la Nyumba ya Mungu, ambapo wadau 2,291 wamepatiwa mafunzo yanayohusu uvuvi endelevu na kushauri jinsi ya kuanzisha vyama vya ushirika vya kukopa na kuweka (SACCOS).

Kufuatia kushamiri kwa uvuvi haramu Wakuu wa Mikoa ya Kilimanjaro na Manyara kupitia vikao vya Kamati za Ulinzi na Usalama waliamua kuanzisha kikosi kazi (Task Force Team) kilichoshirikisha wadau wote ili kupanga na kusimamia mikakati ya kupambana na uvuvi haramu. Hatua hiyo inafuatia operesheni maalum iliyoendeshwa na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi mwezi Mei, 2009.

Mabwawa ya kufugia samaki yameongezeka kutoka 75 yaliyokuwepo hadi kufikia mabwawa 1009 yenye uwezo wa kuzalisha tani 401.6 kwa mwaka. Mkoa umefanikiwa kuanzisha kituo cha kuzalisha vifaranga maeneo ya Kileo, wilaya ya Mwanga ambapo mabwawa 3 yenye wastani wa ukubwa mita 45 x mita 60 yenye uwezo wa kuzalisha zaidi ya vifaranga 18,000yameanzishwa. Vifaranga zaidi ya 6000 vimeshasambazwa katika mkoa wa Kilimanjaro kutoka mabwawa haya na vingine kutoka Gereza la Karanga.

Halmashauri za wilaya za Rombo, Mwanga na Moshi zimetenga Shs.23.0 Million kupitia mipango ya maendeleo ya kilimo ya wilaya (DADPs) kwa ajili ya kuimarisha shughuli za uvuvi katika Halmashauri zao



Moja ya mabwawa ya kufugia samaki Wilayani Rombo.

9.2 Changamoto:

Sekta ya uvuvi inakabiliwa na changamoto kubwa kama ifuatavyo:-

i) Kushamiri kwa uvuvi haramu hasa katika Bwawa la Nyumba ya Mungu unasababisha uharibifu wa mazalia ya samaki na uvuvi wa samaki wadogo. Uvuvi huu unasababisha upungufu mkubwa wa samaki katika Bwawa hili ambao umefikia wastani wa tani 510 badala ya uwezo wa bwawa wa kuzalisha zaidi ya tani 5100.

ii) Kuwepo kwa mabadiliko makubwa ya tabianchi yanasababisha kina cha maji kupungua mwaka hadi mwaka na hivyo kuathiri mabwawa ya uzalishaji samaki.

iii) Ongezeko kubwa la wananchi kandokando ya maziwa na hivyo kuathiri mazingira kufuatia shughuli za kiuchumi wanazozifanya hasa zile za kilimo kisichokuwa endelevu.

iv) Upungufu wa wataalam wa sekta ya uvuvi na vitendea kazi ambapo mkoa una wataalam 16 badala ya idadi ya 34 wanaohitaji, na pikipiki 2 na boti 2 badala ya angalau pikipiki 20 na boti 5 ziendazo kwa mwendo wa kasi.

9.3 Matarajio:

Mkoa katika kuboresha na kuendeleza sekta ya uvuvi unategemea:-

i) Kuendelea kutoa elimu kwa wadau wote juu ya uzalishaji samaki na uvuvi endelevu.

ii) Kuboresha na kuwezesha uzalishaji vifaranga wa samaki kutoka wastani wa vifaranga 18,000 kwa mwaka hadi kufikia vifaranga 100,000 hadi ifikapo mwaka 2015.

iii) Kushughulikia suala la upungufu wa wataalam na vifaa vya kufanyia kazi.

iv) Kuendelea kuboresha misitu na vyanzo vya maji kwa kupanda miti na kuzuia shughuli za kibinadamu kwenye vyanzo vya maji.

10.0 Ushirika

Vyama cha Ushirika mkoani Kilimanjaro vimekuwa sehemu muhimu ya maendeleo ya mkoa huu kwa miaka zaidi ya sabini na tano (75) sasa. Vuguvugu la uanzishwaji wa vyama vya ushirika lilianzia pale wakulima wa kahawa walipopata matatizo ya uuzaji wa zao la kahawa kupitia wafanyabiashara wa kati (walanguzi wa ki-Asia) na hivyo kupelekea uamuzi wa kuunda umoja wao uliojulikana kama "**Kilimanjaro Native Planters Asssociation**" - (KNPA) mwaka 1925. Mwaka 1932 serikali ya wakati huo iliamua kutunga Sheria ya Vyama vya Ushirika nchini na ilipofika tarehe 29 Desemba, 1933 "**Kilimanjaro Native Co-operative Union**" - (KNCU) kiliandikishwa na kuwa chama kikuu cha ushirika cha kwanza Afrika kikiwa kimeundwa na vyama vya msingi kumi na kimoja (11) kutoka iliyokuwa wilaya ya Kilimanjaro.

Vyama vya Ushirika vya KNCU na Vuasu vimekuwa na mchango mkubwa wa maendeleo ya mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla. Vyama hivi vimewezesha wakazi wa Kilimanjaro kusomesha watoto wao kutokana na na uuzaji wa mazao yao kwa bei nzuri. Vyama hivi viliweza kuanzisha shule kwa ajili ya kusomesha watoto wa wakazi wa Kilimanjaro. Mfano wa shule iliyoanzishwa na vyama vya ushirika ni Lyamungo sekondari iliyoanzishwa na KNCU.

Katika kuimarisha ushirika wa walaji katika Mji wa Moshi na vitongoji vyake, mwaka 1962 Chama Cha Ushirika cha Walaji "Moshi District Consumers Cooperative Society Ltd" kilianzishwa na kimeendelea kufanya kazi hadi sasa. Mwaka 1964 vyama 40 zaidi vilikuwa vimeandikishwa na kufanya idadi ya vyama vya msingi vya mazao chini ya KNCU kuwa 50. Chama Kikuu cha Ushirika VUASU kiliandikishwa tena mwaka 1963 katika wilaya ya Pare kikiwa kimeundwa na vyama 15 vya Ushirika vya Msingi vya Mazao.



Mgahawa wa kisasa unaomilikiwa na (KNCU) baada ya kukarabatiwa mwaka 2010

Aidha Chuo cha Ushirika kilicholenga kufundisha Wataalam na wafanyakazi katika sekta ya ushirika kilianzishwa Moshi mwaka 1964 ambacho kimekua na kufikia Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara mwaka 2009.



Jengo la Utawala la Chuo Kikuu cha Ushirika na Stadi za Biashara (MUCCOBs)

Sekta ya Ushirika katika Mkoa wa Kilimanjaro ilikuwa na mafanikio makubwa kama ifuatavyo:-

(i) Idadi ya vyama vya Ushirika vya msingi imeongezeka kutoka vyama 96 mwaka 1961 hadi 421 mwaka 2011

(ii) Idadi ya wanachama imeongezeka kutoka wanachama 36,762 mwaka 1961 hadi 259,178 mwaka 2011.

(iii) Mtaji umeongezeka kutoka 240,000/= mwaka 1961 hadi kufikia sh. 6,729,263,540/= mwaka 2011.

(iv) Hapakuwepo na Benki za Ushirika mwaka 1961 lakini kufikia mwaka 2011 zimeanzishwa benki mbili ambazo ni"Kilimanjaro Cooperative Bank" na "Mwanga Community Bank".

10.1 Changamoto:

Uchache wa wanachama unaopelekea mitaji na uwezo wa kiuchumi kuwa mdogo. Mwaka 1976 serikali ilifuta vyama vya ushirika vya mazao vijijini na vyama vikuu vya ushirika na hivyo kusababisha matatizo/ changamoto za kimuundo na za kiuendeshaji ambayo iliathiri maslahi ya vyama vya ushirika.

10.2 Matarajio:

Ushirika kuwa chombo muhimu kitakachosaidia mkoa kufikia lengo la uchumi wa kisasa unaojitegemea kwa kuwafundisha watendaji, viongozi na wanachama wenyewe stadi za uendeshaji vyama vya ushirika katika mfumo wa soko huru. Aidha, kuimarisha uandishi wa vitabu vya hesabu, ufungaji wa hesabu na ukaguzi wa hesabu na mali za vyama vya ushirika.

11.0 MAZINGIRA NA UTALII (1961-2011)

11.1 Misitu ya Asili (Misitu ya lindi Maji)

Wakati Tanzania Bara inapata Uhuru, serikali ya kikoloni ilikuwa imeshaanzisha sheria za kulinda na kuhifadhi misitu, maeneo ya wanyamapori, hifadhi ya mazingira na vyanzo vya maji. Mkoa wa Kilimanjaro ulikuwa na maeneo 20 tofauti ya hifadhi yenye ukubwa wa hekta 143,000 yaliyokuwa yamehifadhiwa kama ifuatavyo:-

Na	Jina la Hifadhi/Msitu	Ukubwa (Ha)	Mmiliki
	Chome	14,283	Serikali kuu
	Chambogo	5467	Serikali kuu
	Mwala	1373	Serikali kuu
	Kwamwenda	583	Serikali kuu
	Koko Hill	78.1	Serikali kuu
	Vumari	1829.24	Halmashauri
	Kwizu	3070	Halmashauri
	Gonja	70.82	Halmashauri
	Madanda	8.33	Halmashauri
	Chongweni	92.27	Halmashauri
	Mramba	3355	Serikali kuu
	Minja	520	Serikali kuu
	Kamwala I & II	1 – 117 II - 293	Serikali kuu
	Kindoroko	885	Serikali kuu
	Kahe I	885	Serikali kuu
	Kahe II	202	Serikali kuu
	Rau	570	Serikali kuu
	Kiverenge	1758.35	Serikali kuu
	Kileo	191	Halmashauri
	Msitu wa asili unaozunguka mlima Kilimanjaro	107	Serikali kuu

Msitu unaozunguka mlima Kilimanjaro ambao ndio chanzo kikuu cha mito inayotiririsha maji ulianza kuhifadhiwa kwa Sheria Na.389 ya mwaka 1958. Kufuatia umuhimu wa msitu huu ulipandishwa hadhi na kuwa Hifadhi (Catchment Forest) mwaka 1975. Mlima Kilimanjaro umekuwa kivutio kikubwa cha watalii wanaopanda mlima tangu Mzee Lauwo alipofanikiwa kuwapandisha watalii na kuwafikisha katika kilele cha mlima kazi anayoendelea nayo hadi leo.

Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro ilipandishwa hadhi kuwa Hifadhi ya Taifa mwaka 2005 na baadaye kutangazwa na Umoja wa Mataifa (UNEP) kuwa eneo la urithi wa dunia (World Heritage Site) mwaka 1989. Kabla ya kupata Uhuru kulikuwepo na hoteli za kitalii 2 tu za Livingstone Hotel na KNCU ambazo zilikuwa zinatoa huduma kwa wazungu hasa watalii, Waasia na viongozi.

Serikali ya kikoloni kwa kutambua umuhimu wa kuhifadhi miti ya asili, ilianzisha mashamba mawili kwa ajili ya kupanda miti katika maeneo ya Rongai na West Kilimanjaro ili kuzalisha miti ya mbao kwa shughuli za ujenzi. Mashamba haya yalianzishwa mwaka 1954 kwa shamba la Rongai lenye ukubwa wa Ha.6400 na shamba la West Kilimanjaro lenye ukubwa wa Ha.6,800.

11.2 Mabadiliko ya Sera na Sheria za kuhifadhi Misitu

Kufuatia uharibifu mkubwa wa mazingira ulioambatana na ukataji miti ovyo, uchomaji wa misitu na kilimo kisichozingatia hifadhi ya mazingira mwaka 1998 Serikali iliamua kutunga sera na sheria mpya zilizokuwa na lengo la kufanyia mapitio sheria zilizokuwepo kabla ya kupata Uhuru. Sheria mpya ya misitu Na.14 ya mwaka 2002 na kanuni zake za mwaka 2004 zinasisitiza umuhimu wa kuhifadhi misitu na mali nyingine za asili kwa kushirikisha wananchi wanaozunguka maeneo hayo.

Mafanikio:

i) Wakati tunapata uhuru mwaka 1961 hapakuwa na skimu ya uhifadhi wa vyanzo vya maji kutokana na kutokuwepo na uharibifu wa mazingira. Hadi kufikia mwaka 2011 mkoa umeanzisha skimu 259 za uhifadhi wa vyanzo vya maji.

ii) Matumizi ya mizinga ya nyuki yameongezeka kutoka mizinga ya asili iliyokuwepo mwaka 1961 hadi kufikia mizinga ya kisasa 4,747 mwaka 2011.

iii) Uzalishaji wa asali umeongezeka kutoka kilo 300 mwaka 1961 hadi kilo 34,965 mwaka 2011.

iv) Hadi mwaka 2011 jumla ya miti 2,026,000 ilikuwa imepandwa.

v) Halmashauri zote zimetunga sheria ndogo za kudhibiti mazingira. Aidha mkoa umezuia uchafuzi wa mazingira katika miji. Tabia za kujisaidia hovyo na utupaji hovyo wa taka umedhibitiwa.

vi) Hoteli zimeongezeka kutoka hoteli 2 za kitalii (Livingstone hotel na KNCU) mwaka 1961 hadi hoteli 41 mwaka 2011.

vii) Idadi ya watalii imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka mwaka hadi kufikia watalii 40,709 mwaka 2011.

viii) Idadi ya hifadhi za taifa zimeongezeka kutoka 0 mwaka 1961 hadi 2 mwaka 2011 (Kilimanjaro na Mkomazi). Wanyamapori k.m. vifaru, walikuwa wengi baada ya Uhuru ila hali hii ni kinyume miaka 50 baada ya Uhuru vifaru wamekuwa wachache sana.



Msitu wa Hifadhi ya Rongai.

12.0 VIWANDA NA BIASHARA

12.1 Viwanda:

Mwaka 1961 kilikuwepo kiwanda kimoja tu cha TPC Ltd cha kutengeneza sukari. Kiwanda cha TPC Ltd kilianzishwa mwaka 1930 na kampuni moja ya Denmark na kilisajiliwa nchini Denmark kwa jina la (Tanganyika Planting Company Limited - TPC Ltd). Kampuni hii ilisajiliwa nchini Tanzania tarehe 29 Juni 1973 kwa jina hilo la TPC Ltd, na wamiliki walikuwa hao hao wa awali, yaani M/S A.P. Moller wa Denmark




Mashine za kusaga na kusindika Tangawizi Mamba Miamba wilayani Same.

Kwa mara ya kwanza, kampuni hii ilizalisha sukari tani 4,000 kwa mwaka 1936 kutokana na miwa iliyolimwa na kuvunwa Arusha Chini. Miaka 50 baada ya uhuru, kiwanda cha TPC Ltd kinazalisha sukari tani 86,000 (2010/11) kwa mwaka na kinamilikiwa kwa ubia kati ya serikali ya Tanzania na kampuni ya M/S Sukari Investment Company Ltd ya Maurtius.

Hadi kufikia mwaka 2011, viwanda vimeongezeka hadi 130 vinavyoajiri zaidi ya wafanyakazi 7,311 vikiwemo vikubwa 19 vya kati 25 na vidogo 86. Viwanda hivi vinajihusisha zaidi na usindikaji wa mazao ya kilimo, mifugo na misitu; utengenezaji wa dawa mbalimbali; vyombo vya nyumbani, vinywaji na vifungashio.

Katika kipindi cha 1995 – 2002 serikali ilibinafsisha baadhi ya mashirika ya umma, vikiwemo viwanda, katika kutekeleza sera ya ubinafsishaji. Viwanda vya umma vilivyobinafsishwa mkoani Kilimanjaro ni pamoja na kiwanda cha magunia Moshi, kiwanda cha ngozi, kiwanda cha dawa za kilimo, kiwanda cha sukari TPC Ltd na viwanda vya mbao – Kilimanjaro Timber Utilization Co. Ltd na Imara Wood Products Ltd.



Rais Nyerere akikata utepe kufungua rasmi kiwanda cha ngozimjini Moshi 1968

Viwanda vilivyobinafishwa vinaendelea kuzalisha isipokuwa Kiwanda cha Magunia Moshi, Kiwanda cha Dawa za Kilimo na kiwanda cha Kilimanjaro Machine Tools Limited. Serikali inaendelea na mikakati mbalimbali ya ufufuaji wa viwanda hivi vilivyofungwa ikiwa ni pamoja na kutafuta na kukaribisha wawekezaji wenye uwezo.

12.2 Uwekezaji:

Mwaka 1961 hapakuwepo na mazingira mazuri yaliyovutia uwekezajiukilinganisha na hali ilivyo baada ya miaka 50 ya Uhuru. Katika miaka 50 ya uhuru mazingira ya kuvutia uwekezaji yameboreshwa kwa ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ifuatayo:-

- Ujenzi wa barabara 2,596.47 zilizohitimisha mkoa kuwa na jumla ya kilomita 3,646.07 mwaka 2011 za barabara nzuri kutoka kilomita 1,049.6 zilizokuwepo mwaka 1961
- Ujenzi wa miundombinu mzuri ya kukidhi huduma ya maji safi na salama kwa asilimia 72 mwaka 2011 kutoka asilimia 11 mwaka 1961
- Ujenzi na uboreshaji wa miundombinu na teknolojia ya mawasiliano kutoka simu chache za mezani mwaka 1961 hadi mwaka 2011 kutumia simu za mikononi, tovuti,mtandao 'internet' na kompyuta.
- Ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya upatikanaji na usambazaji wa nishati.
- Idadi kubwa ya wananchi wenye elimu kukidhi haja ya teknolojia mbalimbali za uwekezaji.
- Ujenzi na uboreshaji wa mtandao wa viwanda,biashara na usambazaji kwa kiwango cha kukidhi haja ya mahitaji mbalimbali.
- Ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya kuvutia utalii ikiwa ni pamoja na misitu, hifadhi mbalimbali za wanyama, hoteli za kitalii n.k.
- Kuwa na sera na sheria zinazokidhi mahitaji ya wawekezaji.
- Kuwa na taasisi nyingi za fedha zinazokidhi haja za wawekezaji.
- Ujenzi wa mazingira mazuri na ya kuridhisha ya ulinzi na usalama.
- Ujenzi na uboreshaji wa masoko ya mpakani (Rombo) na hivyo kuongeza wigo wa kufaidi fursa za masoko zinazotokana na mtangamano wa jumuia za kikanda za Jumuia ya Afrika Mashariki 'EAC' na Jumuia ya nchi huru kusini mwa Afrika 'SADC'.
- Kuwa na kituo cha uwezekaji mkoani kinachoendeshwa chini ya sheria ya uwekezaji Tanzania namba 26 ya mwaka 1997.

12.3 Matarajio:

Kutokana na kuboreshwa kwa mazingira ya uwekezaji yaliyotajwa juu, na pia kutokana na mlima mrefu kupita yote barani Afrika kuwa mkoani Kilimanjaro ambao ni kivutio kikubwa cha utalii mkoani pote, ni matarajio makubwa fursa nyingi za uwekezaji mkoani Kilimanjaro katika sekta mbalimbali zitaendelea kunufaika zikiwa ni pamoja na **utalii, kilimo, mifugo, viwanda, elimu, afya na nishati.**

13.0 BIASHARA:

Wakati Tanzania Bara (Tanganyika) inapata Uhuru mwaka 1961 biashara nyingi hasa za maduka zilimilikiwa na watu wenye asili ya Asia katika mji wa Moshi na Same. Katika maeneo ya vijiji kulikuwepo na maduka madogo madogo sana na magulio ya kuuza bidhaa na mazao mbalimbali ya chakula.

Mahitaji muhimu kwa wananchi hasa Waafrika yalipatikana kwa shida mfano:-

i) Nguo nzuri, vifaa vya ndani na vifaa vya ujenzi vilipatikana katika maduka machache mjini na vilitumiwa na viongozi na watu wachache waliokuwa na uwezo kiuchumi.

ii) Mashine za kusaga nafaka zilikuwa chache takriban 20 kwa mkoa mzima, hali iliyosababisha wenyeji kutumia mawe ya kusaga unga.

Baada ya Uhuru wananchi wazawa wameendelea kujihusisha katika biashara mbalimbali hadi kufikia mwaka huu 2011, biashara 34,000 zimesajiliwa na mashine za kusaga nafaka zimeongezeka hadi kufikia 600 katika maeneo mbalimbali ya mijini na vijijini.

13.1 Changamoto:

Changamoto inayoendelea kuikabili sekta ya biashara ni pamoja na elimu duni ya ujasiriamali.

13.2 Matarajio:

Mkoa unaendeleza mkakati wa kutoa elimu ya ujasiriamali kwa wananchi wetu ili waweze kuingia kwenye biashara ya ushindani hasa kufuatia kuanzishwa kwa soko huru

la Afrika ya Mashariki. Aidha mkoa unaendeleza mkakati wa kuhamasisha na kuelimisha uboreshaji wa bidhaa zinazozalishwa katika viwanda vyetu ili ziweze kumudu biashara ya ushindani dhidiya bidhaa za nje, hususan nje ya nchi.



Mji wa Moshi unaendelea kujengeka kwa majengo ya kisasa na Hotel za Kitalii kutokana na miundo mbinu mizuri ya uwekezaji**.**

13.3 Mafanikio

- ✓ Kukua kwa biashara na mfumo wa usambazaji kumewezesha wananchi walio wengi kupata huduma na mahitaji muhimu kwa wakati na kwa ubora unaotakikana,
- ✓ Kupata mahitaji na huduma muhimu kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa kumefanya wanchi wajisikie huru na sawa na kuondokana na fikra potofu kuwa ni watu wa matabaka fulani pekee wenye stahiki ya bidhaa ama huduma nzuri,

- ✓ Ukuaji wa mtandao wa biashara na usambazaji umekuza mtandao wa masoko kwa wazalishaji na walaji.

14.0 HUDUMA ZA JAMII

14.1 Elimu:

Mkoa wa Kilimanjaro umepiga hatua kubwa katika suala zima la maendeleo ya elimu. Kabla ya Uhuru mkoa ulikwishapiga hatua ya kuwapatia watu elimu. Jitihada hizo ziliendelezwa hadi nchi yetu ilipopata Uhuru mwaka 1961 na hata miaka iliyoendelea baada ya uhuru. Idadi ya wanaojua kusoma na kuandika imeongezeka kutoka asilimia 38 mwaka 1961 hadi asilimia 95 mwala 2011. Lengo ni mkoa kuendelea kuwa kituo cha utoaji wa elimu bora (centre for Excellence).

14.1.1 Elimu ya Awali:

Madarasa ya elimu ya awali yalikuwepo hata kabla ya kupata uhuru na madarasa hayo yamekuwa yakiongezeka hadi kufikia 857 mwaka 2011 (za serikali 774 na 73 zisizo za serikali). Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995 inasisitiza kuwa kila shule ya Msingi iwe na madarasa ya elimu ya awali na mkoa umekuwa ukihimiza jambo hilo kwa wadau wote wa elimu.

14.1.2 Elimu ya Msingi:

Kama ambavyo Taifa liliridhia kutoa elimu ya Msingi kwa watoto wote wa Kitanzania, mkoa wa Kilimanjaro nao umejihakikishia kuwa unazo fursa za kuwapatia watoto wote Elimu ya Msingi. Elimu hii hutolewa bure katika shule za serikali. Mkoa una fursa za kutosheleza kwa ajili ya kutolea elimu ya msingi kwa watoto wote wenye umri wa kwenda shule (miaka 7 – 13). Hii ina maana kuwa, hakuna mtoto anayekosa fursa ya kusoma katika shule za Msingi.

i) Asilimia ya uandikishaji darasa la kwanza imeongezeka kutoka chini ya asilimia 50 mwaka 1961 hadi asilimia 100 mwaka 2011.

ii) Idadi ya wanafunzi darasa la I – VII imeongezeka kutoka 23,560 mwaka 1961 hadi 303,330 mwaka 2011.

iii) Idadi ya shule za Msingi imeongezeka kutoka 35 mwaka 1961 hadi 933 mwaka 2011 (za serikali 882 na 51 zisizo za serikali).

iv) Idadi ya walimu imeongezeka mwaka hadi mwaka na kufikia walimu 8,782 mwaka 2011.

v) Idadi ya nyumba za walimu imeongezeka mwaka hadi mwaka na kufikia 1,199 mwaka 2011.

vi) Uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi (Book/Pupil Ratio) ulikuwa zaidi ya 1:45 mwaka 1961 na hivi sasa uwiano umefikia 1:3 (2011).

vii) Asilimia ya wanafunzi wanaofaulu na kuchaguliwa kuingia kidato cha kwanza imeongezeka kutoka asilimia 4 mwaka 1961 hadi asilimia 100 mwaka 2011.



Wanafunzi wa shule ya Msingi wakiwa darasani katika moja ya shule mkoani Kilimanjaro

Takwimu za Elimu ya Msingi 2011

NA	HALMASHAURI	IDADI YA SHULE	IDADI YA WALIMU	IDADI YA WANAFUNZI
1	HAI	113	1109	34254
2	MOSHI (V)	267	2732	88310
3	MOSHI (M)	48	690	23240
4	MWANGA	112	767	30435
5	ROMBO	156	1439	53343

6	SAME	184	1357	62781
7	SIHA	53	455	20937
JUMLA		**933**	**8549**	**313,300**



Watoto wenye matatizo ya macho (uoni hafifu) wakijifunza kusoma na kuandika kwa kutumia vifaa maalum katika Shule ya Msingi Same N.A wilayani Same.

14.1.3 Elimu ya Sekondari:

i) Idadi ya shule za Sekondari imeongezeka kutoka 4 (ya serikali 1 na 3 zisizo za serikali) mwaka 1961 hadi 313 mwaka 2011 (za serikali 215 na 98 zisizo za serikali).

ii) Tulipopata Uhuru mwaka 1961 hatukuwa na shule ya kidato cha tano na sita lakini mwaka katika miaka 50 ya Uhuru mkoa umeweza kuwa na shule 59 za A'level (za serikali 19 na 40 zisizo za serikali).

iii) Idadi ya wanafunzi (kidato I-VI) imeongezeka mwaka hadi mwaka na kufikia 133,141 mwaka 2011.

iv) Idadi ya walimu imeongezeka mwaka hadi mwaka kufikia 3,018 mwaka 2011.

v) Hivi sasa kata zote katika mkoa zina shule za sekondari. Baadhi ya kata katika mkoa zina zaidi ya shule moja ya sekondari. Hii inatokana na jamii kuhamasika kujenga shule zaidi za kuweza kuwapokea wanafunzi wote wanaofaulu Mtihani wa kumaliza elimu ya Msingi.

vi) Vipo vituo 18 vya elimu masafa Jumla ya wanafunzi 618 wanajifuza kazi na masomo mbalimbali ya kujiendeleza.

Takwimu za Elimu ya Sekondari 201

NA	HALMASHAURI	IDADI YA SHULE	WAV	WAS	JUMLA
1	HAI	45	7214	8124	15338
2	MOSHI (V)	92	17256	19570	36826
3	MOSHI (M)	27	9415	7758	17173
4	MWANGA	38	8935	8338	17273
5	ROMBO	48	9043	11779	20822
6	SAME	47	10094	10035	20129
7	SIHA	16	2495	3085	5580
JUMLA		**313**	**64452**	**68689**	**133141**

14.1.4 Vyuo:

Idadi ya vyuo vya ualimu vilivyokuwepo wakati tunapata Uhuru mwaka 1961 vilikuwa ni 3 vya serikali na hadi mwaka 2011 vimeongezeka hadi kufikia 7 (vya serikali 3 na 4 visivyo vya serikali). Aidha, wakati tunapata uhuru mwaka 1961 hatukuwa na vyuo vikuu, lakini katika miaka 50 baada ya uhuru mkoa umeweza kuwa na vyuo vikuu 5 (vya serikali 2 na 3 visivyo vya serikali). Idadi ya vyuo rasmi vya ufundi imefikia 71 mwaka 2011 (vya serikali 6 na 65 visivyo vya serikali).

14.1.5 Mafanikio

- Mkoa umeweza kutoa elimu ya msingi kwa wanafunzi wote wenye umri wa kwenda shule kwa makundi yote ya watoto (wenye ulemavu na wasio na ulemavu).
- Zimejengwa shule za sekondari katika kila kata na kuwezesha kila mwanafunzi aliyefaulu kuingia kidato cha kwanza kupata nafasi katika shule zilizopo.
    - ✓ -Pamekuwa na elimu ya ushindani uliowezesha kutoa elimu bora na yenye ushindani **kitaifa na kimataifa** hivyo kufanya baadhi ya wazazi waliokuwa wanapeleka watoto wao nje ya nchi kuacha kufanya hivyo na kuwasomesha katika shule zilizoko mkoani.

14.1.6 Changamoto:

i) Uhaba wa miundo mbinu katika ngazi zote za elimu.

ii) Uhaba wa walimu usioendana na upanuzi wa taasisi za elimu hasa Sekondari.

iii) Jamii kutohamasika ipasavyo katika kupokea miradi mbalimbali ya elimu.

iv) Uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

v) Kufifia kwa shughuli za Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi.

14.1.7 Matarajio:

i) Kuboresha miundombinu ya kutolea elimu na kuongeza idadi ya shule za sekondari zilizopo ili kuwezesha wanafunzi wote wanaofaulu kusoma bila shida

ii) Kuwa na shule za A' level katika kila tarafa,

iii) Kuwa na maabara na nyumba za walimu katika shule zote za sekondari,

iv) Kuinua kiwango cha ufaulu wa shule za Msingi kutoka asilimia 62 hadi kufikia asilimia 100 katika miaka 15 ijayo

15.0 AFYA:

Baada ya Uhuru huduma za afya zilizotolewa zilikuwa za kinga na kutibu maradhi. Huduma za kinga zilitolewa kwa magonjwa ya ndui, kupooza, kifua kikuu, surua, kipindupindu, homa ya manjano na kifaduro, wakati huduma za tiba zilitolewa kwa magonjwa mengine.

Hadi kufikia mwaka 2011 huduma za chanjo za uti wa mgongo na Pneumonia zimeongezeka na viwango vya chanjo kwa watoto wenye umri mwaka mmoja vimepanda kufikia 94% chanjo ya kifua kikuu" BCG", 82% chanjo ya kudhibiti polio kwa mtoto anapozaliwa "OPV0", 90% chanjo ya tatu "OPV3", 90.4% chanjo ya dondaa koo, kifaduro, pepo punda,uti wa mgongo,homa ya mapafu na homa ya ini "DPT-HB + penta" 92% chanjo ya surua, 83% vit A%.



Maabara ya kisasa katika Hospitali ya Mkoa ya Mawenzi.

15.1 Huduma za Tiba:

15.1.1 Zahanati

Zahanati zilizokuwepo baada ya uhuru zilikuwa 60, zimeongezeka na kufikia 341 mwaka 2011. Kati ya hizo za serikali ni 152, Mashirika ya dini 68 na za mashirika ya umma 21.

15.1.2 Vituo vya Afya

Vituo vya afya vilikuwepo ni 3 na mwaka 2011 vipo vituo vya afya 36 kati yake vya serikali ni 22 na mashirika ya dini 5, mashirika ya umma/binafsi 8.

15.1.3 Hospitali

Baada ya uhuru zilikuwepo hospitali 4 zikiwemo za Serikali (Kibong'oto), mashirika ya dini kama vile KCMC na Hospitali ya kampuni ya kiwanda cha TPC. Kwa sasa Mkoa unazo hospitali 19. Idadi inategemewa kuwa kubwa kwani Halmashauri ya Wilaya ya Hai imeanza kujenga Hospitali yake ya Wilaya. Majengo yaliyokamilika ni mapokezi ya nje, kliniki ya uzazi na mtoto, jengo la CTC, jengo la wodi ya watoto, jengo la kuhifadhi maiti, jengo la ufuaji nguo za wagonjwa pamoja na jengo la utawala. Vile vile Halmashauri ya wilaya ya Moshi, Siha, na Hai zimeanza kujenga Hospitali zake za Wilaya, na Manispaa imeingia mkataba na Hospitali ya St. Joseph kuwa Hospitali Teule "DDH". Halmashauri ya wilaya ya Mwanga wamekamilisha ujenzi wa nyumba ya kuhifadhi maiti pamoja na uwekaji wa majokofu.



Ujenzi wa Jengo la wodi ya wazazi katika Hospitali ya Mawenzi Mkoa (Mawenzi).

Hospitali ya Mkoa ya Mawenzi imeendelea kufanyiwa ukarabati katika baadhi ya majengo, na mengine kujengwa upya kama vile jengo la CTC, jengo la upasuaji,

njia za kutembelea, uzio na jengo la kina mama ambalo hivi sasa liko hatua ya ghorofa ya kwanza.

15.1.4 Maradhi ya mlipuko

Jamii yote imeelimishwa juu ya usafi wa mazingira na kuepuka msongamano wa watu, na iwapo mtu atang'atwa na mbwa au paka, n.k. afike kituo cha huduma ya afya mapema.

Katika kipindi hiki mkakati wa kupunguza ugonjwa wa malaria mkoani umefanyika halikadhalika kampeni ya kusambaza vyandarua vyenye viatilifu katika wilaya zote zimefanyika. Shughuli hiyo imefanywa kwa kushirikiana na mashirika ya PSI, MEDA na World Vision.

15.1.5 Uzazi Salama

Mwaka 2005 akina mama waliokuwa wanajifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya walikuwa 60% kufikia mwaka 2010 kiwango kimeongezeka na kufikia 73%.

Kutokana na juhudi za kuboresha huduma za afya, vifo vya watoto wachanga vimeendelea kupungua. Mwaka 2007 vilikuwa 31/1000 na mwaka 2010 vilifikia vifo 23/1000 kati ya watoto waliozaliwa hai.

Aidha, vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano vimeendelea kupungua kutoka **54/1000** wakati tunapata uhuru hadi kufikia vifo **41/1000** kati ya watoto waliozaliwa hai mwaka 2010; na vifo vya wazazi wajawazito vimeendelea kushuka kutoka **124/100,000** mwaka 2006 hadi kufikia **119/100,000** (2010)



Wanakijiji wakiwa katika kituo cha afya cha kijiji wakisubiri huduma ya kiliniki kwa watoto wao Moshi Vijijini.

15.2 UKIMWI

Ugonjwa wa UKIMWI uligundulika hapa Mkoani mwaka 1984, na Serikali ya Mkoa ilichukua jitihada mbalimbali za kukabiliana na tatizo hilo. Jitihada zilizochukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa ni pamoja na kutoa elimu ya kinga kwa wananchi ili kubadili tabia, matumizi ya damu salama na tiba ya kupunguza makali ya UKIMWI inayotolewa kwa wagonjwa.

Kutokana na utafiti uliofanyika maambukizi ya UKIMWI kwa mkoa wa Kilimanjaro yalikuwa asilimia 7.3 mwaka 2009, kiwango hicho kimepungua hadi kufikia asilimia 1.9. Hadi sasa vituo 42 vya kutolea huduma ya dawa za kupunguza makali ya UKIMWI vimefunguliwa na dawa zinatolewa bila malipo kwa wagonjwa wa UKIMWI. Vile vile vituo 231 kati ya vituo vya RCH kliniki 254 hutoa huduma za PMTCT ambazo ni huduma za kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Asilimia 91 ya kiliniki za RCH zinazotoa huduma hii. Kampeni ya Kitaifa ya upimaji VVU ilifanikiwa kwa asilimia 146.

Mkakati wa mkoa ni kuendeleza elimu kwa jamii kuhusu VVU na UKIMWI, kuhamasisha Upimaji VVU kwa hiari, kuzuia maambukizi ya VVU toka kwa mama kwenda kwa mtoto, kutoa tiba ya magonjwa nyemelezi na ufuatiliaji wa wagonjwa majumbani.

15.2.1 Mafanikio:

i) Kiwango cha chanjo kimepanda na kufikia asilimia 89.

ii) Timu ya Usimamizi afya ya mkoa imeweza kupitia Ripoti za robo mwaka na CCHP kila mwaka na Halmashauri zimeweza kupata fedha za kutekeleza mipango yao.

iii) Ongezeko la vituo vya kutolea huduma za afya katika vijiji na kata (MMAM).

iv) Kuwepo kwa jengo la damu salama ambalo hutoa damu salama katika mkoa huu na kanda ya Kaskazini.

v) Kupungua kwa maambukizi ya magonjwa ya ngono hasa kaswende kutoka 3.7% hadi 1%

vi) KCMC kuwa na kliniki ya familia ya kutolea huduma za ARV ambayo kuhudumia familia kwa wakati mmoja badala ya mtu mmoja mmoja.

vii) Kipindi cha nyuma baada ya uhuru halmashauri hazikuwa na maeneo maalum ya kutupia takataka ngumu, lakini kuanzia mwaka 2005 maeneo maalum yanakuwa yakitengwa katika kila wilaya, uzoaji wa taka umeimarika na sheria ndogo zimetungwa na zinatekelezwa ili kudumisha usafi.

viii) Maradhi ya kuambukiza yamepungua kwa kiasi kikubwa.

ix) Usafi wa mazingira umeboreshwa katika wilaya zote. Katika mashindano ya afya na mazingira kitaifa, Manispaa ya Moshi imechukua nafasi ya kwanza kitaifa kwa miaka mitatu mfululizo.

x) Kumekuwa na ongezeko la vyuo vya uuguzi toka 2 (Same na KCMC) hadi 5 (Huruma, Kibosho na Machame).

xi) KCMC imetoa Shahada ya Udaktari, Uuguzi, Maabara na Shahada ya Uzamili katika Afya ya Jamii.

15.2.2 Mafanikio katika mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI:-

i) Maambukizi ya VVU toka kwa mama kwenda kwa mtoto yamepungua toka asilimia 5 hadi asilimia 2.9.

ii) Maambukizi ya VVU miongoni mwa wananchi waliojitokeza kwenye kampeni ya kitaifa ya kupima VVU imepungua toka asilimia 7.3 (2004) hadi asilimia 2.4 (2009)

iii) Magonjwa ya ngono kama kaswende kwa wajawazito imepungua toka asilimia 3 hadi asilimia 1.

iv) Mkoa ulifanikiwa kuvuka lengo la kampeni ya Kitaifa ya upimaji VVU kwa asilimia 146.

v) Huduma za kuzuia maambukizi ya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto "PMTCT" zimesambazwa hadi ngazi ya Zahanati.

vi) Vituo vya kutolea dawa za kupunguza makali ya virus vya UKIMWI 'ARV' vimeongezeka na viko zaidi ya 40 katika ngazi ya hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati kutoka Taasisi za watu binafsi, Mashirika ya dini na Serikali.

vii) Kuanzishwa kwa huduma za kubaini mapema maambukizi ya VVU kwa watoto wanaozaliwa na mama wenye VVU kwa kutumia kipimo maalum cha 'DNA – PCR'.

viii) Unyanyapaa umepungua kwa kiasi kikubwa.

ix) Idadi ya watoa huduma waliopata mafunzo imeongezeka.

15.3 Huduma za mama na mtoto:

i) Jumla ya vituo vya kutolea huduma 254 sawa na asilimia 63.6 vinatoa huduma ya mama na mtoto.

ii) Chanjo kwa watoto asilimia 85.4

iii) Chanjo kwa akina mama asilimia 93.3

iv) Chanjo ya vitamin 'A' kwa watoto asilimia 83.4

v) Chanjo ya vitamin 'A' kwa akina mama asilimia 64

15.4 Changamoto

i) Upungufu wa baadhi ya madawa, vitenganishi na vifaa tiba katika mkoa.

ii) Upungufu wa wafanyakazi katika vituo.

iii) Uchakavu wa miundo mbinu katika hospitali ya mkoa na vituo vingine vya kutolea huduma katika wilaya.

iv) Kitengo cha wagonjwa wa akili kinachohudumia wagonjwa wa kanda ya kaskazini kutokuwa na majengo yanayokidhi mahitaji, wataalam, dawa za kutosha na kutokuwa na bajeti kama kitengo cha kanda.

v) Ushiriki mdogo wa wanaume katika kliniki za uzazi na mtoto.

vi) Upungufu wa dawa za kutibu Kifua kikuu sugu.

vii) Matumizi ya dawa za mitishamba katika kuongeza uchungu kwa baadhi ya mama wajawazito.

viii) Upungufu wa vyombo vya usafiri katika vituo vya huduma.

ix) Uelewa mdogo wa wananchi kuwahi kwenye vituo vya tiba

15.5 Matarajio:

i) Kukamilisha jengo la sakafu nne la wazazi (maternity ward) katika hospitali ya mkoa ya Mawenzi ili kuweza kuongeza idadi ya wakina mama watakaohudumiwa kwa ubora zaidi.

ii) Kukamilisha "Master Plan" kwa msaada wa "ABBOT" ili kutoa nafasi ya ujenzi kwa mpangilio unaovutia.

iii) Kupunguza vifo vya wakinamama wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano.

iv) Kuhakikisha kinamama wanajifungulia kwenye vituo vya kutolea huduma na wanapata huduma hiyo toka kwa wataalam.

v) Kuzidi kuboresha usafi wa mazingira ili kupunguza maradhi ya kuambukiza.

vi) Hospitali ya mkoa kuwa hospitali ya rufaa ili kuongeza huduma bora zaidi kwa wagonjwa na kusogeza huduma karibu na wananchi.

vii) Kujenga chumba cha upasuaji "Theatre" katika vituo vya afya ili kusogeza huduma karibu na wananchi.

viii) Kuboresha huduma maalum za afya kwa ajili ya kuhudumia wazee.

ix) Kuendelea kuratibu tiba mbadala pamoja na tiba asili katika mkoa wetu.

16.0 HUDUMA ZA USTAWI ZA USTAWI WA JAMII

Huduma za ustawi wa jamii hapa Mkoani zilianza kutolewa mara baada ya uhuru wa Tanganyika, na zilikuwa zinatolewa kupitia kitengo kilichojulikana kama "Probation Services" au **Bwana Huruma.** Bwana Huruma alishirikiana na Mahakama kuhakikisha kuwa wale washitakiwa wenye makosa madogo madogo anawaombea msamaha kwa Mahakama ili wapunguziwe adhabu na kuwekwa chini ya uangalizi wa Bwana Huruma kwa kipindi kilichopendekezwa.

Baadaye Miaka ya 1970 ndipo idara kamili ya Ustawi wa jamii ilipoundwa na serikali na shughuli zake kugawanywa katika vitengo vitatu kama ifuatavyo:-

1. Kitengo cha Familia, malezi, Makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto
2. Kitengo cha Majaribio, ujenzi wa tabia na Haki za mtoto/kijana kisheria
3. Kitengo cha Watu wenye ulemavu na wazee

Katika Mkoa Vitengo hivi vilifanya kazi kwa ushirikiano na kuleta tija kwa jamii ambayo inaishi katika mazingira hatarishi ambao kwa ujumla wao walipatiwa huduma nzuri. Hata hivyo idadi ya watumishi waliokuwepo walitosheleza kutoa huduma katika Wilaya ya Moshi Mjini tu ambao walikuwa watumishi wapatao wanne na watumishi wawili katika Mahabusi ya watoto. Mwaka 1969 ofisi ya ustawi wilaya ya Same ilifunguliwa ikiwa na mtumishi mmoja tu, huku ofisi ya ustawi wa jamii Rombo ilifunguliwa mwaka 1977 ikiwa nayo na mtumishi mmoja pia. Wilaya zingine hazikuwa na ofisi ya Ustawi wa jamii hadi hivi karibuni.

NB: Taarifa za utoaji wa huduma za ustawi wa jamii toka mara baada ya Uhuru hadi mwaka 2000 hazikupatika kwa sababu mafaili yote yenye taarifa hizo yalikuwa yametunzwa katika chumba kimoja kilichopo mahabusi ya watoto hapa Moshi ambacho kwa bahati mbaya iliungua moto mwaka 2000.

HUDUMA ZA USTAWI WA JAMII ZILIZOTOLEWA TOKA MWAKA 2001

MASHAURI YA USTAWI WA JAMII YALIYOSHUGHULIKIWA KIMKOA

MWAKA	1	2	3	4	5		6		7	8
					idadi	Watoto	Idadi	Watoto		
2001	928	1000	1580	185	120	14805	10	540	36	0
2002	729	973	1526	310	135	15641	12	685	34	0
2003	906	1066	1496	156	135	15622	16	878	30	0
2004	616	987	1577	133	138	16201	16	896	28	0
2005	950	798	1760	144	136	15978	20	1278	32	0
2006	745	1021	1690	152	140	18924	23	1479	34	0
2007	925	934	1230	131	140	18943	24	1563	30	0
2008	828	749	1104	108	139	18876	26	1742	34	26,121
2009	768	615	1002	136	140	18878	28	1798	28	26,746
2010	896	941	1320	94	140	18921	28	1821	24	26,746

CHANZO: Ofisi ya ustawi wa Jamii (M)

UFUNGUO:

1: Unyumba, **2:** Matunzo, **3:** Mimba nje ya ndoa, **4**: Wajaribiwa (probationers)

5: Day care centres, **6:** Children's homes, **7**: Makazi ya wazee, **8:** Mvcs

Huduma za kuwatambua watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi zilifanyika katika mkoa kuanzia mwaka 2008 ambapo Wilaya/ Halmashauri za Same, Siha, Hai na baadhi ya kata 8 za Halmashauri ya Moshi Vijijini ndizo zilizohusika, hivyo kutoa idadi ya watoto 26,746 (*DMS Ministry of Health and Social welfare*)

16.1 HUDUMA ZA USTAWI WA JAMII 2005-2011:

Katika kipindi hiki (2005-2011) utoaji wa huduma za Ustawi wa Jamii uliongezeka kwa maana ya eneo la utoaji wa huduma (coverage). Mkoa ulipanua huduma za Ustawi wa Jamii kwa kuanzisha ofisi za Ustawi katika Wilaya/Halmashauri za Siha, Mwanga na

Moshi Vijijini ambapo jumla ya maafisa Ustawi wa Jamii wapatao saba (7) waliajiriwa na Halmashauri hizo. Hivi sasa Halmashauri zote saba zinatoa huduma za Ustawi wa Jamii zikiwa na maafisa wapatao 26 kama ifuatavyo:

(i) Manispaa – Maafisa Ustawi wa Jamii 8
(ii) Moshi Vijijini-Maafisa Ustawi wa Jamii 1
(iii) Rombo- Maafisa Ustawi wa Jamii 3
(iv) Siha- Maafisa Ustawi wa Jamii 2
(v) Hai- Maafisa Ustawi wa Jamii 7
(vi) Mwanga- Maafisa Ustawi wa Jamii 2
(vii) Same- Maafisa Ustawi wa Jamii 4

16.2 Huduma ambazo zimeendelea kutolewa ni pamoja na:

(i) Huduma ya familia, matunzo na malezi ya watoto.
(ii) Huduma kwa kwa wazee na watu wenye ulemavu wassiojiweza
(iii) Majaribu,ujenzi wa Tabia na Haki za watoto katika kisheria

Katika awamu hii, 2005-2011, huduma ya matibabu ya bure kwa wazee wasiojiweza imetolewa na hospitali karibu hospitali zote Mkoani na hasa baada ya agizo la Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pia katika kipindi hiki 2005-2011, Halmashauri za Hai, Siha, Same na baadhi ya kata 8 katika Halmashauri ya Moshi Vijijini wameweza kutambua watoto 26,746 wanaoishi katika mazingira hatarishi na kuwapangia mipango kwa ajili ya kuwakwamua katika hali hiyo.

16.3 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA

1. Watumishi wa fani ya ustawi wa jamii kutotosheleza katika Halmashauri zetu
2. Ufinyu wa bajeti unaoikabili serikali na baadhi ya wadau wa utoaji wa huduma hii
3. Baadhi ya wadau kuvamia utoaji wa huduma za ustawi wa jamii bila kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizopo

16.4 MIKAKATI WA UTEKELEZAJI KWA KIPINDI KIJACHO:

Idara ya Ustawiwa Jamii imedhamiria kuboresha utoaji wa huduma za Ustawi wa Jamii katika mkoa kwa kufanya mambo yafuatayo:

- Kuzidi kuwaelimisha Maofisa Ustawi wa Jamii mbinu na mikakati mipya ya utoaji wa huduma kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na wajibu uliopo
- Kuwatambua watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi kwa maeneo/ wilaya zilizobaki na kuainisha mipango thabiti ya kuwakwamua watoto hao.
- Kuwatambua wazee wasiojiweza(60+) ambao wanastahili matibabu ya bure na kisha kuwapatia vitambulisho
- Kuendelea kutoa elimu kwa jamii ili watoto yatima walelewe katika jamii husika/ndugu kuliko kukimbilia kuwapeleka kwenye makao ya watoto ambayo hayakidhi haja.
- Kuendelea kuishauri serikali na wadau ili kuongeza bajeti katika suala zima la utoaji wa huduma za Ustawi wa Jamii mkoani

17.0 MAJI.

Huduma za maji ni muhimu kwa binadamu kwa mahitaji ya afya na maendeleo yake. Katika kipindi cha miaka 50 ya uhuru mkoa umeendelea kusogeza huduma ya maji safi na salama karibu na sehemu wanazoishi wananchi. Katika kipindi hiki jumla ya miradi 190 ya maji ilitekelezwa katika wilaya zote za mkoa wa Kilimanjaro.

17.1 Mafanikio – 1961 hadi 2011:

i) Idadi ya watu wanaopata huduma ya maji safi na salama imeongezeka kutoka 40,000 sawa na asilimia 11 mwaka 1961 hadi 1,119,583 sawa na asilimia 72 mwaka 2011.

ii) Miradi ya maji imeongezeka kutoka 15 mwaka 1961 hadi kufikia 190 mwaka 2011.

iii) Visima virefu na vifupi vyenye pampu vinavyofanya kazi kuanzia mwaka 1961 hadi mwaka 2011 ni 260.

iv) Kati ya vijiji 472, vijiji 438 vina kamati za maji na vijiji 406 vina mifuko ya maji yenye jumla ya shilingi 734,705,313/= hadi 2011**.**

v) Bodi/Mamlaka mbalimbali 17 za kuendesha huduma ya maji zimeanzishwa na kukabidhiwa kwa wananchi kusimamia miradi yao kama vile:-

1) Bodi ya udhamini mradi wa maji Uroki Bomang'ombe.
2) Bodi ya udhamini mradi wa maji Losaa KIA.
3) Bodi ya udhamini mradi wa maji Magadini Makiwaru.
4) Bodi ya udhamini mradi wa maji Lawate Fuka.
5) Bodi ya udhamini mradi wa maji Lyamungo Umbwe.
6) Bodi ya udhamini mradi wa maji Chekereni Weruweru.
7) Kampuni ya Maji KILIWATER na Jumuiya zake saba
8) Jumuiya ya watumia maji Uchira
9) Bodi ya udhamini mradi wa maji Longuo, Rau Karikacha
10) Mamlaka ya maji safi na maji taka Manispaa ya Moshi
11) Mamlaka ya maji safi na maji taka Same Mjini
12) Mamlaka ya maji safi na maji taka Mwanga Mjini
13) Jumuiya ya watumia maji Kilema Kusini
14) Bodi ya udhamini mradi wa maji Kirua Kahe.
15) Jumuiya ya watumia maji Sokoeni
16) Bodi ya udhamini mradi wa maji Machame
17) Bodi ya udhamini mradi wa maji Mkalama.

Idadi ya watu wanaopata maji 2010

Halmashauri	**Idadi ya watu 2002**	**Idadi ya miradi**	**Idadi ya watu 2010**	**Wanaopata huduma 2010**	**Asilimia**
Siha	89,214	5	103,711	72,598	70
Hai	169,721	4	197,301	157,841	80

Moshi	401,369	35	438,080	306,656	70
Mwanga	115,145	33	126,675	70,938	56
Rombo	245,716	20	274,623	205,967	75
Same	211,738	90	240,408	129,820	54
Jumla vijijini	**1,233,903**	**187**	**1,380,798**	**943,820**	**68**
Manispaa Moshi	143,799	3	179,350	175,763	98
Mkoa	**1,376,702**	**190**	**1,563,148**	**1,119,583**	**72**

17.2 Changamoto

i) Uharibifu wa vyanzo na uchafuzi kama vile kulima, kukata miti, kuchoma moto au kuchunga wanyama maeneo ya vyanzo vya maji.

ii) Upungufu wa wataalam katika utumishi wa fani za mafundi mbalimbali wa sekta ya maji, hasa umeme na mitambo.

iii) Kupungua au kukauka kwa vyanzo vya maji vinavyotumika hasa kipindi cha kiangazi na kupungua kwa kiasi cha mvua.(ukame)

17.3 Matarajio

Lengo ni watu wote wapate maji safi na salama katika umbali usiozidi mita 400 au muda usiozidi dakika 30 kwenda na kurudi kutoka kwenye makazi yao ifikapo 2025. Aidha wananchi watahamasishwa kujenga matanki ya kuvuna maji ya mvua pamoja na kutunza vyanzo vya maji kwa kupanda miti, kuzuia uchafuzi na kuweka mipaka ili kudhibiti uharibifu ili upatikanaji wa maji safi na salama uwe endelevu.

18.0 MIUNDOMBINU

18.1 Barabara:

Mkoa wa Kilimanjaro una mtandao wa barabara wenye jumla ya kilomita 3,646.07. Mtandao wa barabara unaohudumiwa na Wizara ya Miundombinu kupitia Wakala wa Barabara (TANROADS) ni kilomita 974.27 ambapo Barabara Kuu ni kilomita 295.34 na barabara za mkoa ni kilomita 678.93 mwaka 2011. Baada ya uhuru barabara zilikuwa katika madaraja ya "Territorial Main" (Barabara Kuu), "Local Main" (Barabara za Mkoa), "District Roads" (Barabara za wilaya) na "Unclassified Roads" au "Feeder Roads" na matengenezo ya barabara yalikuwa chini ya Wizara ya Mawasiliano. Hivi sasa barabara nyingi ziko chini ya halmashauri za wilaya/manispaa.



Barabara ya lami katika eneo la Rongai wilayani Rombo.

Mtandao wa barabara umeongezeka kutoka km 1,049.6 mwaka 1961 hadi 3,646.07 mwaka 2011 zikiwa katika mchanganuo ufuatao:

Barabara za lami	km.	443.88
Barabara za changarawe	km.	1,440.12
Barabara za udongo	km.	1,762.17
Jumla	km.	**3,646.07**

18.2 Hali ya barabara ni kama ifuatavyo;-

- Kilometa 846.74 (22.22%) zina hali nzuri
- Kilometa 1632.45 (44.77%) zina hali nzuri wastani
- Kilometa 1167.01 (32.01%) ziko katika hali mbaya.

Mtandao wa barabara za Hamashauri/Manispaa umeongezeka kutoka Km. 1049. hadi Km 2,923.87 kama ifatavyo:

Barabara za lami	Km 87.40
Barabara za changarawe	Km 850.50
Barabara za udongo	Km 1,985.97
Jumla	**Km.2,923.87**

Hali ya mtandao wa barabara za halmashauri za wilaya/manispaa ni kama ifuatavyo:

- Barabara zenye hali nzuri 22.62%
- Barabara zenye hali nzuri ya wastani ni 42.0%
- Barabara zenye hali mbaya ni 35.4%

Ujenzi wa barabara mpya katika utekelezaji wa ahadi za Rais



Mkuu wa Mkoa Mhe. Monica N. Mbega akizindua ujenzi wa barabara ya Kibosho Road – Kwa Rafael kwa kiwango cha Lami, tarehe 03.05.2010





Kazi ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kwenye barabara za mkoa, mwaka 2010/2011

18.3 Changamoto:

i) Wakandarasi wengi wa kazi za barabara wa daraja la tano, sita na saba ambao ndio wanaofanya kazi nyingi za halmashauri hawana mitambo muhimu ya kazi za barabara. Kazi nyingi huchelewa kukamilika kwa sababu ya uhaba wa mitambo na uchakavu wa mitambo inayopatikana.

ii) Halmashauri zina uhaba wa watumishi wa Sekta ya Miundombinu, tatizo linalochangia kuchelewa maandalizi ya zabuni za barabara na pia kutowepo usimamizi wa karibu wa kazi za matengenezo ya barabara.

iii) Kutokana na uhaba wa ardhi barabara nyingi za halmashauri hazina maeneo ya akiba inayoweza kutumika kujenga mirefeji ya maji ya mvua.

iv) Kutokuwepo sheria ndogo za halmashauri kusimamia kutengwa maeneo ya hifadhi ya barabara na kuyalinda.



Muonekano wa barabara ya iliyojengwa chini ya kiwango cha changarawe ikipita katika milima ya Ugweno bara hii inapitika katika majira yote ya mwaka.

18.4 Matarajio

Barabara zote za vijijini kuwa kwenye hali nzuri kwa asilimia 100 ifikapo 2025, na barabara zote za mijini kuwa za lami na kuwekwa taa.

18.5 Mawasiliano

Wakati tunapata uhuru mawasiliano yalikuwa kwa njia ya simu za mezani kwa kutumia Shirika la Posta na Simu kwa maeneo machache hasa ya mjini. Simu za mkononi hazikuwepo. Hadi kufikia mwaka 2005, mtandao wa simu za mkononi ulikuwa unapatikana maeneo yote ya Mkoani. Kampuni zinazotoa huduma ni Vodacom, Tigo, Zain, TTCL na Zantel. Vile vile mwaka 2005 hayakuwepo mawasiliano ya mtandao (internet), lakini hivi sasa Mkoa na Halmashauri zote zina mawasiliano ya internet. Aidha mkoa umefanya maandalizi yakuunganishwa na mkongo wa Taifa na hivyo mawasiliano yataboreka zaidi. Taarifa na vifurushi kwenda maeneo tofauti zilitumwa kwa njia ya posta au usafiri wa gari/gari moshi

na ndege. Teknologia imeendelea kwa kasi na mwaka 2011 mawasiliano yanafanyika kwa kompyuta na taarifa zinatumwa kwa mtandao (internet).

18.6 Changamoto

Elimu juu ya Teknolojia ya habari na mawasiliano kwa wananchi ni ndogo na inabadilika kwa kasi siku hadi siku; na hivyo kuhitaji mafunzo na kozi za mara kwa mara ili kuongeza ujuzi wa kukabiliana na mabadiliko hayo.

Miundombinu ya mawasiliano kuboreshwa na teknolojia mpya ya kisasa ya usafirishaji wa mtandao (fiber optic cable) kusambaza mtandao katika Halmashauri zote. Kila Halmashauri iwe na Tovuti (Website) inayowekwa taarifa mpya mara kwa mara na kutoa taarifa mbalimbali kwa wananchi na wadau. Hivi sasa Mkoa una tovuti yake www.kilimanjaro.go.tz. Vile vile kuwa na chumba maalumu cha kuendesha 'electronic conference' ijulikanayo kama 'Video conference' ya Mkoa.

19.0 Sekta ya Ardhi:

Katika kipindi cha miaka 50 sekta ya Ardhi imesimamia masuala ya Mipango Miji, Upimaji na Ramani hifadhi ya kumbukumbu ya milki ya Ardhi, usimamizi na umilikishaji Ardhi na utatuaji wa migogoro ya Ardhi. Mkoa umeanzisha miji midogo minne ya **Himo, Same, Mwanga na Hedaru** baada ya ukuaji wake kufikia hatua za kuendelezwa kimipango Miji. Upanuzi wa miji kwa ujumla wake ni mgumu kutokana na uhaba mkubwa wa Ardhi unaokabili mkoa wa Kilimanjaro, na wananchi wake kutokuwa tayari kuachia maeneo yao kwa ajili ya upanuzi wa miji. Mfano Halmashauri ya Manispaa Moshi imeshindwa kupanua mipaka yake ili iweze kufikia hadhi ya kuwa Jiji.

19.1 Maendeleo ya Miji/Miji Midogo:

Miji imeongezeka kutoka mji mmoja wa Moshi wakati tunapata uhuru hadi kufikia zaidi miji saba ambayo ni Moshi Manispaa, Himo, Mwanga, Same, Bomang'ombe, Sanya Juu, na Mkuu Rombo .Aidha kuna miji mingine midogo katika wilaya zetu kama Hedaru, Kisiwani, Makanya, Holili, Tarakea, Ndungu, Kihurio n.k

19.2 Upimaji wa Viwanja Mijini:

Kila halmashauri imefanya jitihada binafsi za kupima viwanja katika miji ya wilaya na miji midogo kwa ubunifu tofauti, kama vile kutumia bajeti za halmashauri na kushirikisha nguvu za wananchi kuchangia gharama, na kukopa kwenye mfuko wa upimaji viwanja mijini "Plot Development Revolving Fund – PDRF".

19.3 Upimaji wa Mipaka ya Vijiji:

Mwaka 2005 mkoa ulikuwa na vijiji 433 vilivyosajiliwa. Mwaka 2011 vijiji vimeongezeka na kufikia vijiji 472 kwa mujibu wa tangazo la serikali Na.205 na 205A la mwaka 2009 na Nyongeza Na.9 Vol.91 ya mwezi Mei mwaka 2010.

Katika kipindi cha 2005 – 2010 mipaka ya vijiji 434 vilipimwa kama ifuatavyo;-

	Same	**Rombo**	**Mwanga**	**Hai**	**Siha**	**Moshi**	**Jumla**
Idadi ya Vijiji	91	65	71	61	39	145	**472**
Vijiji vilivyopimwa	78	60	60	54	37	145	**434**

19.4 Upimaji wa Mashamba na mipaka ya Hifadhi ya Taifa:

Upimaji wa mashamba unafanyika kwa kasi ndogo sana kwa kuzingatia uhaba wa ardhi uliopo mkoani hapa, ambapo mashamba 89 yamepimwa. Aidha upimaji wa mipaka ya Hifadhi za Taifa za Mlima Kilimanjaro (KINAPA) na Mkomazi umefanyika ikiwa ni pamoja na kutenganisha **"half mile strip"** na wananchi.

19.5 Milki ya Ardhi:

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imefungua ofisi ya Kamishna Msaidizi wa Ardhi Moshi kwa ajili ya kuhudumia Kanda ya Kaskazini. Kwa sasa hati zinatayarishwa na halmashauri kisha zinakaguliwa na kuidhinishwa na Kamishna wa Ardhi Msaidizi. Hatua hii imepunguza usumbufu wa wananchi kufuata huduma hiyo Makao Makuu ya Wizara Dar es Salaam. Katika kipindi hiki jumla ya hati 3,623 zimetayarishwa.

19.6 Migogoro ya Ardhi:

Katika mkoa huu migogoro mingi ya ardhi inachangiwa na uhaba mkubwa wa ardhi pamoja na taratibu za kumilki ardhi kimila (vihamba). Hata hivyo Wizara ya Ardhi imefungua Baraza la Ardhi na Nyumba katika Wilaya za Moshi na Same. Kesi nyingi zinazoshindikana kusuluhishwa katika Mabaraza ya Vijiji na Kata ambayo yako katika kila kijiji na kata hupelekwa katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya.

19.7 Orodha na taarifa za Mabaraza ya Ardhi ya Kata na Vijiji:

HALMASHAURI	MABARAZA YA ARDHI		PASIPO NA MABARAZA		MASJALA YA ARDHI		MABARAZA YALIYOPATA MAFUNZO	
	KATA	VIJIJI	KATA	VIJIJI	KATA	VIJIJI	KATA	VIJIJI
HAI	10	55	-	-	-	-	-	-
SIHA	4	37	-	-	-	-	-	-
ROMBO	20	60	-	-	-	-	20	60
SAME	25	83	6	8	-	-	-	-
MWANGA	16	60	-	-	-	1	-	-
MOSHI (V)	31	145	-	-	-	3	-	-
MOSHI MANISPAA	15	0	6	-	-	-	-	-
JUMLA	**121**	**440**	**12**	**8**	**0**	**4**	**20**	**60**

19.8 Changamoto:

i) Uhaba wa ardhi unafanya juhudi za kupanua miji kuwa ngumu.

ii) Watumishi wa sekta ya ardhi wanatumia muda mwingi kusuluhisha migogoro ya ardhi.

iii) Elimu ya sheria za ardhi haijawafikia wananchi walio wengi, hii inasababisha wananchi wasifahamu haki zao.

iv) Hati za kimila hazitambuliwi na vyombo vya fedha (Mabenki) pale wananchi wanapotaka kutumia hati hizo kama dhamana.

19.9 Matarajio:

i) Kuimarisha mabaraza ya ardhi ya Vijiji na Kata ili yaweze kutatua migogoro ya ardhi kwa ufanisi zaidi.

ii) Kuanzisha na kuimarisha masijala ya ardhi katika ngazi ya vijiji.

iii) Kuimarisha ofisi za vijiji ziwe na hadhi inayostahili na ziwe na ukumbi wa mikutano.

19.10 Changamoto za jumla

i) Ubinafsishaji wa viwanda ambavyo vimeacha kuzalisha

ii) Msongamano wa watu unaotokana na uhaba wa ardhi

iii) Ukame

iv) Kasi ya uharibifu wa mazingira unaotokana na mabadiliko ya tabia ya nchi

v) Upungufu wa watumishi katika sekta mbalimbali za umma

vi) Ongezeko la magugumaji katika ziwa Jipe

19.11 Hitimisho

Tumethubutu kufanya na yaliyofanyika yanaonekana. Uongozi uliotangulia umetuonesha njia na mafanikio haya yatakuwa chachu ya kufanya mazuri zaidi katika kuleta maendeleo ya mkoa wetu wa Kilimanjaro.

Awamu Nne za utawala wa Serikali na vyama vilivyotuongoza tangu tupate uhuru (TANU na CCM), zimeweza kutekeleza Ilani za Uchaguzi za vyama hivyo na kutuwezesha kupiga hatua ya kufikia mafanikio haya tunayojivunia. Kutekelezwa

kikamilifu kwa Ilani ya Uchaguzi ya chama tawala kutawezesha mkoa wetu kupiga hatua kubwa zaidi za maendeleo na kuwa mfano mzuri kwa mikoa mingine; na hivyo kuwezesha maisha bora kwa kila mwananchi.

INAWEZEKANA KILA MTU AKITIMIZA WAJIBU WAKE KIKAMILILIFU

"TUMETHUBUTU, TUMEFANYA, TUMEWEZA NA TUNAENDELEA KUSONGA MBELE"